SportPesa
TZS.804,667,160
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



UKURASA 4

## RIPOTI MAALUM

Simulizi ya mwanafunzi aliyebakwa na mchunga ng'ombe kwenye kichaka



ama
ALHAMISI DESEMBA 23, 2021
AFYA NA MAZINGIRA

Ukurasa 12
Shinyanga vitani kujichomoa kutoka kundi vinara maradhi Ukimwi kitaifa

Ukurasa 13
UNALIFAHAMU HILI?
Kila utajiri mazingira unaojinasibu nao unashikiliwa na hazina misitu

SALAMU ZA UN 2022
Janga corona liwe darasa haja ya uwekezaji mkubwa kiafya

Na Mwandishi Wetu

IKIWA ni muda mfupi kuingia mwaka mpya 2022, huku dunia ikitishwa na janga jipya la maradhi corona, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Dk. Antonio Guterres, anaitaka dunia kutumia janga corona na vita vyake kuwa kigezo muhimu kwa serikali zote kuwekeza zaidi katika mifumo imara ya afya.

Katika ujumbe wake kuhusu Siku ya Kimataifa ya Huduma za Afya kwa Wote inayoadhimishwa Desemba 12 ya kila mwaka, anasema mifumo hiyo ndiyo itaweza kumlinda kila mtu kwa sasa na vizazi vijavyo.



UKURASA 11

Alhamisi Desemba 23, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580803

www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Wagonjwa corona waongezeka nchini

**KATI** ya vifo 10, saba hawakuchanja. Watanzania 80,000 kupata chanjo kila siku... *Endelea ukurasa 2*

UKURASA WA 3

## ACT KUKUSANYA MAONI TUME HURU YA UCHAGUZI

UONGOZI wa ACT-Wazalendo umeiagiza ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa chama hicho kukusanya maoni ya wanachama kuhusu....



UKURASA WA 3

## GEREZA LAELEMEWA NA WAFUNGWA, MAHABUSU

GEREZA la Wilaya ya Shinyanga la Mhumbu, limeelemewa na msongamano wa wafungwa na mahabusu, hivyo kusababisha...

UKURASA WA 3

## FAMILIA MHITIMU WA SUA YASEMA INAMWACHIA MUNGU

FAMILIA ya mhitimu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Magreth Mashue (26), aliyeuawa na watu wasiojulikana na mwili wake kutupwa kwenye mashamba ya chuo...



Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam wakinunua bidhaa mbalimbali ikiwamo nguo katika Mtaa wa Kongo jana, ikiwa ni maandalizi ya Sikukuu ya Krismasi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Serikali yailipa PSSSF bilioni 500/- za mafao

UKURASA 2



Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba (kulia), akibadilishana mkataba na Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Hosea Kashimba (kushoto), katika hafla ilifanyika jijini Dodoma jana. Anayeshuhudia ni Mwanasheria Loveness Msechu wa Wizara ya Fedha na Mipango. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Aliyelala kitandani aamka yuko kwenye mti

UKURASA 9

MICHEZO SIMBA: TUMEFUATA POINTI TATU TABORA UK.24 MAONI, KATUNI UK.6

# Maambukizi corona yaongezeka nchini

**Na Mary Geofrey,** ARUSHA

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, amesema maambukizi ya UVIKO-19 yanaongezeka nchini, hivyo wananchi wanatakiwa kuendelea kuchukua tahadhari.

Ametolea mfano idadi ya sampuli zinazopokewa Maabara Kuu za Taifa ni 47 kwa siku, tofauti na awali zilipopokewa sampuli 14 kwa siku, hali inayoonyesha idadi ya maambukizi inaongezeka.

Dk. Gwajima alibainisha hayo jana jijini Arusha wakati wa uzinduzi wa Kampeni ya Uhamasishaji na Utoaji wa Chanjo ya UVIKO-19 katika Mpango Harakishi na Shirikishi Awamu ya Pili, unaotekelezwa na Wizara ya Afya kupitia Kitengo cha Elimu kwa Umma.

Alisema katika kuelekea kipindi cha sikukuu za mwisho wa mwaka, kuna uwezekano wa maambukizi kuongezeka kutokana na watu kuendelea kushiriki shughuli zenye mikusanyiko. Dk. Gwajima alisema wananchi wamekuwa hawachukulii suala hilo kwa uzito unaotakiwa na ndio sababu hawaendelei kuchukua tahadhari. "Kasi ya kujikinga na maambukizi bado ni ndogo. Licha ya kuwa wananchi wanaendelea kuchanja, bado wanahitaji msukumo," alisema Dk. Gwajima.

Akizungumzia hali ya wagonjwa wa UVIKO-19, alisema kati ya wagonjwa 10 wanaofariki dunia, saba kati yao ni wale ambao hawajachanja na wengine watatu ni wale waliochanja, lakini waliozidiwa na magonjwa mengine kama shinikizo la damu, kisukari na wazee. "Tunataka tusikilizane, kila mtu achukue tahadhari na serikali haitaki kutumia nguvu kuwasihi wananchi na kutoa makatazo ya kusherehekea sikukuu, bali jamii inatakiwa kuchukua tahadhari zote," alisema.

Waziri huyo alisema serikali imeendelea kutekeleza wajibu wake kwa kuhakikisha upatikanaji wa chanjo, kuweka miongozo mbalimbali na Rais Samia ameweka mazingira mazuri ya wadau kuendelea kulisaidia taifa kupata chanjo nyingi zaidi.

Sambamba na hilo, alitaja mikoa mitano inayofanya vizuri katika utoaji wa chanjo na mitano inayofanya vibaya katika mpango huo. Alisema mikoa inayoongoza kwa kufanya vizuri katika utoaji wa chanjo ya UVIKO-19 ni Ruvuma, Mwanza, Dodoma, Kagera na Mara.

Alitaja mikoa mitano inayofanya vibaya katika utoaji wa chanjo ya UVIKO-19 ni Manyara, Njombe, Singida, Iringa na Songwe.

Waziri huyo aliwataka viongozi wa mikoa inayofanya vibaya kutimiza wajibu wao wa kumsaidia Rais Samia katika majukumu aliyowapatia katika maeneo hayo.

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongela, alisema suala la chanjo limefanikiwa kwa sababu ya msimamo wa Rais Samia ambaye alisimamia kuhakikisha chanjo zinaingia nchini.

Alisema Wizara ya Afya nayo inasimamia vyema utekelezaji huo na viongozi wengine ngazi ya chini. Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Adam Malima, alisema walifanya tathmini katika mkoa huo wiki iliyopita kuangalia awamu ya kwanza ya mpango huo ulivyofanikiwa.

Alisema walibaini kuwapo kwa mafanikio na sasa katika kutekeleza awamu ya pili, wamejipanga kuutekeleza kwa kushirikisha viongozi wa serikali za mitaa, vijiji, vitongoji na viongozi wa dini na kimila.

Alisema wale wote ambao hawajaingia katika mpango huo wa chanjo, waungane na kupata chanjo ili kuendelea kuwakinga Watanzania dhidi ya maambukizi.

**MAREKANI YATOA DOZI NYINGINE MIL. 1.6**

Tanzania jana imepokea shehena nyingine ya zaidi ya dozi milioni 1.6 ya chanjo dhidi ya UVIKO-19 aina ya Pfizer BioNTech zilizotolewa na Serikali ya Marekani kupitia Mpango wa Kimataifa wa Usambazaji chanjo wa COVAX.

Msaada huo ulipokelewa rasmi na Kaimu Meneja wa Programu ya Kinga na Chanjo kutoka Wizara ya Afya, Dk. Ngegwe Bulula, kutoka kwa Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID) nchini, Kate Somvongsiri, katika hafla fupi iliyofanyika katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere.

Kama sehemu ya jitihada zake za kulitokomeza janga hilo duniani, hadi hivi sasa Serikali ya Marekani imeipatia Tanzania zaidi ya dozi milioni tatu za chanjo dhidi ya UVIKO-19. Shehena ya kwanza kutoka Marekani iliyohusisha zaidi ya dozi milioni moja za aina ya Johnson and Johnson ilipokelewa mwezi Julai na kuiwezesha Tanzania kuzindua kampeni ya kitaifa ya chanjo dhidi ya virusi vinavyosababisha UVIKO-19.

Mwezi Novemba, Serikali ya Marekani ilitoa dozi 500,000 za chanjo aina ya Pfizer BioNTech ili kusaidia zaidi jitihada za Tanzania za kukabiliana na kusambaa kwa UVIKO-19.



Ofisa Mkuu wa Fedha wa Benki ya NMB, Juma Kimori, akimkabidhi tuzo ya NMB kuwa Benki Salama zaidi Tanzania kwa mwaka 2021, Kaimu Ofisa Mkuu Udhibiti na Utekelezaji wa benki hiyo, Oscar Nyirenda, tuzo hiyo imetolewa na Jarida la Glob Finance la nchini Marekani. Kulia ni Mkuu wa Idara ya Wateja Maalum, Getrude Mallya na Mkuu wa Idara ya Hazina, Jeremia Lyimo (kushoto). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yaipatia PSSSF bil. 500/- kulipa mafao wastaafu

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

SERIKALI imesema imelipa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) Sh. bilioni 500 kati ya Sh. bilioni 724 inazodaiwa.

Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba, alibanisha hayo jana wakati wa utiaji saini wa makubaliano ya ulipaji Sh. trioni 2.17 kati ya serikali na PSSSF jijini hapa.

Alisema kutokana na hali hiyo hategemei kupata malalamiko ya madai ya mafao kutoka kwa wanachama wa mifuko ya hifadhi ya jamii baada ya kutiwa saini kwa hati hiyo fungani.

Tutuba alisema mpaka sasa serikali imeshalipa mfuko huo Sh. bilioni 500 kati ya Sh. bilioni 724 ilizokuwa inadaiwa kwenye uhakikiki wa mwisho uliofanyika.

"Nia ya serikali ni kuona wastaafu ambao wamelitumikia taifa letu wanafurahia maisha yao ya ustaafu, hivyo baada ya kutia saini makubaliano yetu, ni matarajio yetu kuwa malalamiko kutoka kwa wanachama yatapungua,"alisema.

Katibu Mkuu aliahidi kuwa serikali itaendelea kulipa deni hilo ili kuhakikisha mfuko huo pamoja na sekta ya hifadhi ya jamii inakuwa na ustawi ili kulinda maslahi ya wadau kwa muda mrefu ujao.

Alibanisha kuwa makubaliano yaliyofikiwa na kutiwa saini yataongeza ufanisi na utendaji wa mfuko hasa katika kuwahudumia wanachama ambao wengi wamestaafu baada ya kulitumikia taifa.

Tutuba pia aliitaka mifuko ya hifadhi ya jamii kuendelea kujipanga vyema ili kuhakikisha inawalipa wanachama wanaostaafu kwa wakati.

Mkurungenzi Mkuu wa PSSSF, Hosea Kashimba, alisema wameendelea kulipa pensheni ya kila mwezi kwa wazee na wanalipa mafao ya Sh. bilioni 60 kila mwezi.

Kashimba alisema mkataba uliotiwa saini utakuwa na thamani ya Sh. trilioni 4.66 ambao kwa kuanzia utaruhusu serikali kutoa hati fungani zisizo taslimu za thamani ya Sh. trioni 2.17 za muda wa kuanzia miaka minane hadi 25 kwa mfuko. Alibanisha kuwa uwekezaji huo utasaidia mfuko kupata mapato yanayotokana na hati fungani hiyo ambapo takriban Sh. bilioni 120 kwa mwaka zitapatikana. Kadhalika, alisema kila kiasi kitakachopokelewa kitaelekezwa kwenye maeneo kusudiwa ikiwemo uwekezaji ili kuongeza thamani ya ukwasi wa mfuko.

Mkurugenzi Mkuu huyo alisema PSSSF imefungua ofisi za kanda pamoja na kuanzisha huduma mbalimbali kwa lengo la kuwasogezea huduma wanachama na waajiri popote walipo na wakati wowote. Aliongeza kuwa huduma ya PSSSF kiganjani zitamwezesha mwanachama kufahamu taarifa za uchangiaji wake na taarifa za malipo ya pensheni kwa wastaafu pamoja na mwanachama kupata mrejesho wa maswali mbalimbali.

# Watu 80,000 kupatiwa chanjo corona kila siku

**Na Mary Geofrey,** ARUSHA

KATIBU Mkuu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Prof. Abel Makubi, amesema Mpango Harakishi na Shirikishi Awamu ya Pili wa Kampeni ya Uhamasishaji na Utoaji Chanjo ya UVIKO-19 unalenga kuchanja watu 80,000 hadi 100,000 kwa siku.

Amesema kila mkoa utatakiwa kuchanja watu 4,000 hadi 5,000 kwa siku ili kuwafikia watu wengi zaidi na kufikia lengo la kuchanja asilimia 60 ya Watanzania.

Prof. Makubi alibainisha hayo jana katika uzinduzi wa Kampeni ya Kuelimisha na Kuhamasisha Chanjo ya UVIKO-19 katika Mpango wa Harakishi na Shirikishi Awamu ya Pili, uliofanyika viwanja vya Ngarenaro jijini Arusha.

Mpango huo unaotekelezwa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kupitia Kitengo cha Elimu kwa Umma.

Alisema kuwa katika awamu ya kwanza ya mpango huo walikuwa wakichanja watu 20,000 hadi 40,000 kwa siku na ndio sababu ya kuanzisha mpango huo harakishi na shirikishi.

"Mpango huu utahusisha mitaa na nyumba kwa nyumba na pamoja na kuhamasisha chanjo, wataalamu wa afya watatoa huduma za kupima na matibabu kwa wagonjwa waliopatikana na magonjwa," alisema.

Mtendaji huyo wa wizara alisema utafiti unaonyesha asilimia 70 ya Watanzania wako tayari kuchanja chanjo ya UVIKO-19.

Alisema kuwa kwa upande wa Afrika, utafiti unaonyesha pia asilimia 70 hadi 80 wako tayari kupata chanjo ya UVIKO-19.

Aliongeza kuwa wameanza kufanya utafiti wa chanjo wa UVIKO-19 na magonjwa mengine nchini.

Prof. Makubi alisema Wizara ya Afya pia inaendelea kutoa elimu kwa jamii ili ielimike na kuanza kuelimishana wenyewe katika kudhibiti maambukizi ya ugonjwa huo.

Alisema serikali imetumia mfumo wa afya na serikali za mitaa kuhakikisha elimu inawafikia moja kwa moja wananchi na kupata chanjo.

"Kupitia elimu inayotolewa watu wanaelimika bila kufunga mipaka ya nchi na shughuli za uchumi zinaendelea," alisema Prof. Makubi.

Alisema awamu ya kwanza ya mpango huo ilifanikisha watu kujitokeza kwa wingi kupata chanjo na kusababisha chanjo za Johnson & Johnson kumalizika kwa wakati.

Alisema kwa sasa kuna aina mbili za chanjo na wananchi waendelee kuchanja.

"Hatua hii inaonyesha kuwa Rais Samia (Suluhu Hassan) anawapenda Watanzania na kuwaona wananchi wanakuwa na afya njema, tumefanya kuwa harakishi kwa sababu ugonjwa wenyewe ni haraka na unaua watu kwa haraka," alisema Prof. Makubi.

# ACT kukusanya maoni Tume Huru ya Uchaguzi

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa ACT-Wazalendo umeiagiza ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa chama hicho kukusanya maoni ya wanachama kuhusu Tume Huru ya Uchaguzi wanayoitaka.

Katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, alibainisha hayo jana alipokutana na kuzungumza na viongozi wa chama hicho kutoka Jimbo la Nyasa, ikiwa ni sehemu ya ziara yake katika mikoa ya kichama ya Ruvuma, Mtwara, Selous, Lindi, Pwani na Tanga.

Alisema chama hicho kimeliweka kipaumbele suala la Tume Huru ya Uchaguzi ili kuhakikisha uchaguzi mkuu mwaka 2025 na wa serikali za mitaa kwa mwaka 2024 unakuwa huru, haki na wenye kuaminika.

"Kwenye kikao cha wadau wa siasa juu ya hali ya demokrasia nchini kilichofanyika Dodoma, suala la Tume Huru ya Uchaguzi liliafikiwa na pande zote.

"Kwetu sisi ACT-Wazalendo, hatua inayofuata ni mjadala wa kitaifa kuhusu aina ya tume huru tunayoihitaji," alisema Shaibu.

Aliongeza kuwa vikao vya ACT-Wazalendo kupitia (Kamati Kuu ya mwezi Juni na Halmashauri Kuu ya mwezi Oktoba 2021) viliagiza chama kuweka kipaumbele suala la Tume Huru ya Uchaguzi.

Shaibu pia alibainisha kuwa mbali na maoni ya wanachama, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa chama hicho iliagizwa kufanya rejea ya uzoefu wa mataifa mengine yenye tume huru za uchaguzi zinazopigiwa mfano pamoja na ripoti mbalimbali ikiwamo Rasimu ya Tume ya Jaji Warioba.

Kiongozi huyo wa ACT-Wazalendo yuko kwenye ziara hiyo kwa lengo la kuendesha harambee ya kuchangisha michango ya kugharamia Mkutano Mkuu wa chama unaotarajiwa kufanyika Januari 29 mwakani pamoja na kufafanua mageuzi ya uendeshaji chama kisayansi yanayotarajiwa kuzinduliwa kwenye mkutano mkuu huo.

Jana, Shaibu alikuwa mkoani Mtwara kwenye Jimbo la Songea Mjini.



Mkurugenzi wa Hazina wa Benki ya CRDB, Alex Ngusaru (kulia), akimkabidhi kadi ya gari mshindi wa kampeni ya Simbanking "Mzigo Promosheni" kwa Novemba, Victor Danford Mbulingwe, mkazi wa Dar es Salaam kupitia tawi la Benki ya CRDB Kijitonyama, jijini Dar es Salaam. Kutoka kushoto Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi, Stephen Adili, Meneja wa Benki Kijitonyama, Rosemary Nchimbi na Meneja wa Benki Kanda ya Mashariki, Badru Idd. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Familia mhitimu SUA aliyeuawa yasema yote inamwachia Mungu

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

FAMILIA ya mhitimu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Magreth Mashue (26), aliyeuawa na watu wasiojulikana na mwili wake kutupwa kwenye mashamba ya chuo, imesema inamwachia Mungu kwa kuwa ndiye mwamuzi wa kila jambo.

Wakati familia ikitoa kauli hiyo, mamia ya wanafunzi wa chuo hicho, jana walijitokeza katika viwanja vya chumba cha kuhifadhia maiti katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro, kwenye ibada ya kuaga mwili wa mhitimu huyo.

Akizungumza baada ya ibada ya kuuaga mwili, dada wa marehemu, Liliani Mashuwe, alisema mazishi yanatarajia kufanyika leo katika kijiji cha Shimbikati Kata ya Mkuu, Rombo mkoani Kilimanjaro.

Lilian alisema familia imepokea kwa masikitiko makubwa kifo cha ndugu yao, hivyo wanaachia mamlaka husika kufuatilia tukio hilo na kwamba taratibu zote kwa ajili ya mazishi zimeshafanyika kijijini kwao.

"Tunasikitika kwa sababu hatukutegemea kifo cha ndugu yetu kitakuwa cha namna hii, lakini yote ni mipango ya Mungu. Baada ya kumaliza kuaga tutasafiri hadi kijijini kwetu Shimbikati kwa ajili ya mazishi siku ya kesho (leo)," alisema.

Magreth aliyehitimu chuoni humo Novemba 26, mwaka huu, na kutunukiwa Shahada ya Sayansi ya Mazingira, alitoweka Desemba 14 na kuokotwa na wanakijiji Desemba 18, mwaka huu.

Akiongoza ibada ya kuuaga mwili wa marehemu, Mchungaji wa Kanisa la Tanzania Assemblies of God TAG, Buza, Dismal Kimario, aliwataka ndugu wa marehemu kumshukuru Mungu kwa kila jambo kama maandiko ya Biblia Takatifu yanavyosema.

Mchungaji Kimario alisema Wakristo wanaamini kila jambo hupangwa na Mungu na kwamba kitu pekee kilichobaki kwa ndugu, marafiki na jamaa zake ni kusali na kumwombea apumzike kwa amani na kuziachia mamlaka husika kufuatilia ili sheria ichukue mkondo wake.

"Kama maandiko yanavyotuelekeza tushukuru kwa kila jambo, tunaamini kijana wetu safari yake ndiyo imeishia hapa kwa mipango yake haijalishi chanzo bali Mungu ndiye ameamua kumchukua. Tuendelee kumwombea kwa Mungu apate pumziko la milele," alisema.

# Gereza laelemewa na wafungwa, mahabusu

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

GEREZA la Wilaya ya Shinyanga (Mhumbu), limeelemewa na msongamano wa wafungwa na mahabusu na kusababisha uhaba wa malazi.

Mkuu wa Gereza hilo, Wiliam Makwaya, alibainisha hayo jana wakati Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, alipokuwa akikabidhi magodoro 50 kwa ajili ya wafungwa na mahabusu.

Alisema gereza hilo kwa sasa linakabiliwa na msongamano mkubwa wa wafungwa na mahabusu, ambao hufika hadi 450 huku likiwa na uwezo wa kubeba watu 160.

"Gereza letu Wilaya ya Shinyanga tunakabiliwa na msongamano mkubwa wa wafungwa na mahabusu na kusababisha ukosefu wa malazi, uwezo wetu ni kubeba watu 160, lakini tunafikisha hadi 450 hali ambayo ni hatari kiafya," alisema Makwaya.

Akizungumza wakati wa kukabidhi magodoro hayo, Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, kwa Mkuu wa Magereza mkoani humo, Lazaro Nyanga, alisema wametoa msaada huo ili kutatua tatizo la malazi kwenye magereza hiyo.

Alisema licha ya wafungwa kuwa ni wakosaji, haimaanisha kwamba wakose haki zao za msingi kwa kuwa ni binadamu kama wengine na wamo gerezani kwa ajili ya kupata mafunzo ya makosa yao, ndiyo maana serikali ina hakikisha ina linda usalama na afya zao.

"Magodoro haya 50 ambayo nayakabidhi katika magereza hii ya wilaya ya Shinyanga, nimeyapata kutoka Kampuni ya GSM, kuna mengine yatakuja 50 na kufika 100, lengo ni kutatua changamoto ya malazi kwenye magereza ili wafungwa na mahabusu wawe sehemu salama," alisema Mjema.

Kwa upande wake Mkuu wa Magereza, Nyanga, alimshukuru Mkuu huyo wa Mkoa kwa kufanikisha upatikanaji wa magodoro ambayo yatasaidia kupunguza tatizo la malazi kwa wafungwa na mahabusu.

# Simulizi mwanafunzi aliyebakwa na mchunga ng'ombe kichakani

## ■Alinusurika kuliwa na fisi alfajiri

**Na Elizabeth Zaya**

ALICHANA nguo yangu ya ndani, akatimiza haja zake. Dakika chache za kubakwa na yule mchunga ng'ombe zikakatisha ndoto zangu za kielimu," Bahati (si jina lake halisi) anasimulia mkasa wa ukatili na chanzo cha kufukuzwa shuleni.

Bahati (22), mkazi wa Kijiji cha Mang`weta wilayani Mpwapwa mkoani Dodoma, anaendelea kusimulia kwa undani mkasa huo wa miaka sita iliyopita, akitamka:

"Sikuwahi kufikiri kwamba na mimi lingenitokea hili, nilikuwa ninasikia tu kwa watu wengine. Nikiwa na umri wa miaka 15 mwaka 2015 wakati ninatoka shuleni, kipindi hicho nilikuwa kidato cha tatu katika Shule ya Sekondari Namweta hapa Mpwapwa.

"Nikiwa na wadogo zangu wawili wa kidato cha kwanza siku hiyo, saa kumi na mbili na nusu jioni, giza lilikuwa limeanza kuingia, ilikuwa siku ya michezo shuleni na ndio siku tuliyokuwa tunachelewa sana kutoka kwa sababu mimi pia nilikuwa ninashiriki michezo.

"Ilikuwa siku ya Ijumaa, tarehe sikumbuki ila ilikuwa Julai mwaka 2015. Siku hiyo mvua ilikuwa imenyesha. Tulipofika kwenye Mto Mang`weta, maji yalikuwa yameongezeka. Ikabidi niwavushe wale wadogo, nilianza wa kwanza nikamvusha vizuri, wa pili naye nikamvusha. Baada ya hapo nikawa ninanawa tope miguuni.

"Baada ya kumaliza kunawa, nikawa ninaondoka, wadogo zangu walikuwa wametangulia mbele kidogo. Ghafla nikasikia kuna mtu anaita 'wee binti', alikuwa nyuma yangu.

"Nikageuka na kumwona ni kijana mmoja hivi ambaye mara nyingi tulikuwa tukimkuta anachunga ng`ombe maeneo yale. Nilimuuliza 'unasemaje?' huku nikiongeza mwendo, alikimbia na kuja kusimama mbele yangu.

"Aliniambia 'leo sikuachi'. Yule kijana alinishika kwa nguvu, nikawa ninajaribu kujinasua lakini alinizidi nguvu akanivutia kwenye kichaka. Nilipiga kelele lakini wale wadogo zangu hawakusikia. Wakati ninapambana naye akanipiga kichwani, akanichania na nguo yangu ya ndani kunibaka kisha akakimbia."

Bahati anasema kuwa wakati mchungaji ng'ombe anakimbia, aliendelea kupiga kelele ili kupata msaada kwa wapita njia lakini hakufanikiwa, akilazimika kutembea polepole huku akilia.

"Wadogo zangu niliwakuta kwa mbele sana wakiwa wamekaa chini wananisubiri wakati huo ninalia. Waliponiuliza niliwaambia 'kuna mtu amenipiga na nimewaita hamwitiki'. Niliamua kuwaficha maana nilijua ni aibu na pengine wangesema kijijini au shuleni na ningeweka wapi sura yangu," anasema.



Anaendelea kusimulia kuwa hata alipofika nyumbani kwa wazazi wake, hakuwaambia kilichojiri dhidi yake na ilibaki siri yake mpaka miezi michache baadaye alipogundulika kuwa na ujauzito.

"Ilipita miezi mitatu sijauona mwezi (kupata hedhi), ikabidi nijipime mwenyewe, nikagundua nilikuwa na ujauzito, nilichanganyikiwa, nikawa nalia kila siku, nilikosa raha mpaka mama yangu alipogundua na ndipo niliamua kumsimulia kilichonikuta mpaka kufikia hali hiyo.

"Mama yangu pia alichanganyikiwa, niliendelea kwenda shuleni mpaka ujauzito ulipofika miezi saba, tulipopimwa wasichana wote shuleni na nikagundulika. Na siku hiyo tulibainika wasichana wanne, tukawa tumefukuzwa wote mwaka 2016.

"Mkuu wa Shule alikuja hadi nyumbani kuuliza nini kimenikuta kwa sababu nilikuwa nafanya vizuri shuleni. Akamshauri mama yangu aniendeleze nikijifungua lakini mama hakuwa na uwezo huo, nikaendelea kukaa nyumbani na mtoto wangu," Bahati anasimulia kwa simanzi.

Katika udadisi wake kuhusu maisha ya Bahati shuleni, Nipashe ilibaini kwamba kijana huyo wakati anahitimu elimu ya msingi katika

> "Aliniambia 'leo sikuachi'. Akanishika kwa nguvu... akanichania nguo ya ndani..."

Shule ya Msingi Mseta Bondeni wilayani Mpwapwa, alikuwa miongoni mwa wahitimu 24 na miongoni mwa 18 waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza.

Ufuatiliaji wa Nipashe pia ulibaini kuwa wahitimu wote 18 waliochaguliwa kujiunga na elimu ya sekondari katika shule moja na wakati wakiwa kidato cha kwanza mwaka 2013, wanafunzi wenzake 17 waliacha kwenda shuleni kutokana na sababu mbalimbali, kubwa ikiwa umbali mrefu waliokuwa wakitembea kuifikia shule kutoka nyumbani.

"Ni kweli shida tulizokuwa tunazipitia zilikuwa nyingi. Mbali na kikwazo cha mto, tulikuwa tunachoka sana maana kutembea ni saa mbili kutoka nyumbani hadi kufika shuleni na humo njiani tulikuwa tunakutana na mambo mengi, kama hivyo kusumbuliwa na wachunga ng`ombe na bodaboda.

"Na ukichelewa kuingia darasani unachapwa viboko, na usipokazana sana unaweza kushika hata nafasi za chini sana kwenye mtihani.

"Hata hivyo, pamoja na kwamba wenzangu wengi tuliotoka pamoja shule ya msingi waliamua kuacha shule, niliamua kubaki shuleni, wazazi na walimu walinitia moyo kwamba nisikate tamaa, wakaninunulia na baiskeli ili nisiogope," Bahati anasema.

### BAA LA FISI

Bahati anasimulia mkasa mwingine uliompata akiwa katika safari yake hiyo ya maisha ya shule, akikumbusha kuwa baada ya kununuliwa baiskeli, aliamini ilikuwa mwisho wa matatizo yake, lakini akiwa anatumia usafiri huo, alinusurika kuliwa na fisi wakati akielekea shuleni.

"Ninakumbuka siku hiyo nilikuwa ndio kwanza nimevuka mto, ile napanda tu baiskeli kuendelea na safari, nikaona majani yanatikisika. Kuangalia vizuri nikamwona fisi anapenya kuja njiani, nilikimbiza baiskeli, akawa ananifuata.

"Bahati nzuri nikasikia mlio wa pikipiki mbele yangu, nikaongeza mwendo wa baiskeli, fisi naye hakati tamaa anakuja tu, kumbe aliyekuwa kwenye hiyo pikipiki ni mwalimu wangu alikuwa anakwenda kijijini, nikamwambia ageuze kuna fisi nyuma yangu.

"Kabla ya kugeuza, akaanza kupiga honi kwa fujo, tukaona fisi amekimbilia porini, ikabidi mwalimu naye arudi na mimi mpaka shuleni," Bahati anasimulia.

### SAA TATU ZA KUTEMBEA

Kimsingi, udadisi wa Nipashe wilayani Mpwapwa umebaini kwamba kisa cha Bahati kinashabihiana na madhila yanayowapata wanafunzi wengi wanaosoma katika shule za sekondari na msingi ambazo kuzifikia ni lazima kuvuka mito.

Baadhi ya wanafunzi wamekuwa wakilazimika kuacha kwenda shuleni mito inapojaa hasa kipindi cha masika.

"Hapa umekuta mto hauna maji, ungekuja kipindi cha masika ungetuonea huruma. Wakati mwingine natoka nyumbani alfajiri lakini inachukua saa moja kufika hapa mtoni.

"Ukifika hapa unakuta mto umejaa maji na kama unavyoona ulivyo mpana, nashindwa kuvuka. Inabidi nirudi, wale vijana wanaovusha ni gharama kubwa Sh. 3,000 kwa wanafunzi na Sh. 5,000 kwa wakubwa," mmoja wa wanafunzi anamsimulia mwandishi aliyelazimika kuongozana naye hadi eneo hilo ili kupata picha halisi ya kinachowasibu wanafunzi.

Mwanafunzi huyo pamoja na wenzake watano (mmoja wa kiume) wanaosoma katika Shule ya Sekondari Matomondo waliongozana na mwandishi wa Nipashe wakitembea kwa miguu kutoka Kijiji cha Mbori kuelekea shuleni kwao, ikichukua takriban saa moja na nusu kuufikia Mto Mamba.

Kinachoshuhudiwa mtoni, wanafunzi wanavua viatu kabla ya kuvuka kisha kuvivaa wanapofika ng'ambo na safari inaendelea, ikichukua takriban saa moja na nusu tena kuifikia shule yao.

Mmoja wa wanafunzi hao anayesoma kidato cha tatu, anasema ni kawaida kwake kuwakuta wenzake wameshaingia darasani na mara nyingi hukikosa kipindi cha kwanza.

"Muda wa kuingia darasani ni saa mbili asubuhi labda kuwe na shughuli nyingine ya muhimu ambayo wanafunzi wanafanya ndio wanachelewa kuingia, lakini sisi mara nyingi tunachelewa, na tulishawaambia walimu wanajua tatizo letu ila kuna siku huwa wanatuchapa, wanasema tunachelewa sana, hilo la kuchelewa vipindi ni kawaida kwetu, hasa cha kwanza," anasema.

ITAENDELEA KESHO

# MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001:2015

# TANGAZO KWA UMMA

## UHUISHAJI WA LESENI ZA UZALISHAJI BIDHAA ZINAZOTOZWA USHURU WA BIDHAA / DENATURED SPIRITS

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapenda kuwakumbusha wazalishaji na wanaotarajia kuanza uzalishaji wa bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa au spiriti yenye vionjo (denatured spirits) kuwa, leseni za mwaka 2021 zilizotolewa chini ya kifungu Na. 8 na/au 16 cha Sheria ya Usimamizi wa Ushuru wa Bidhaa (Excise (Management & Tariff) Act) Sura ya 147, zinatarajiwa kufikia ukomo wa matumizi mnamo tarehe 31 Desemba 2021. Hivyo basi, wazalishaji wanakumbushwa kuleta maombi kwenye Ofisi za TRA ili kuhuisha leseni zao kwa ajili ya mwaka 2022 na kuepuka usumbufu unaoweza kujitokeza mara baada ya leseni zao za sasa kufikia ukomo.

**Masharti ya Leseni;**

i). Maombi yapelekwe Ofisi ya TRA iliyo karibu kwa kutumia Fomu Na. **ITX258.01. E** inayopatikana kwenye tovuti ya TRA (www.tra.go.tz) na kwenye ofisi za TRA nchi nzima. Fomu za maombi ziwasilishwe kwenye ofisi ya TRA ya mwombaji.

ii). Maombi tofauti yatafanywa kwa kila kiwanda kinachojihusisha na uzalishaji wa bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa pamoja na kila kundi la bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa.

iii). Leseni itatolewa kwa mwombaji husika, na itatumika katika kiwanda husika na itatumika kuzalisha bidhaa iliyopewa leseni pekee.

iv). Sigara na tumbaku iliyoboreshwa vitahesabika kama kundi moja la bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa.

v). Mzalishaji mwenye leseni hatoruhusiwa kuihamisha leseni husika, kiwanda au kutengeneza bidhaa iliyo kwenye kundi jingine (different class of excisable goods) bila kuomba na kuruhusiwa na Kamishna Mkuu.

vi). Leseni itatolewa baada ya kuwasilishwa kwa ushahidi wa malipo ya ada ya maombi ya leseni ya shilingi Laki Tano (500,000/=) kama ilivyotajwa katika Kanuni ya 4 ya Kanuni za Leseni na Usimamizi wa Wazalishaji wa Bidhaa Zinazotozwa Ushuru wa Bidhaa na/au Spiriti zenye vionjo (Denatured Spirits) za mwaka 2020

Ifahamike kuwa, kwa mujibu wa Kifungu Na. 8 na 16 cha Sheria ya Usimamizi wa Ushuru wa Bidhaa (Excise (Management & Tariff) Act) Sura ya 147, ni makosa kuzalisha bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa au spiriti yenye vionjo bila ya kuwa na leseni halali inayotolewa na Kamishna Mkuu. Kosa hilo linaweza kupelekea adhabu ya faini au kifungo au vyote kwa pamoja. TRA itaendesha ukaguzi wa kina kubaini wazalishaji wa bidhaa husika wanaoendesha shughuli zao bila ya kuwa na leseni halali na kuwachukulia hatua stahiki.

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

**Imetolewa Na;**
**MKURUGENZI WA HUDUMA NA ELIMU KWA MLIPAKODI**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tusherehekee sikukuu kwa amani, tahadhari

**JUMAMOSI** ni Sikukuu ya Krismas kwa Wakristo kote duniani kukumbuka siku ya kuzaliwa kwa mwokozi wao Yesu Kristo, katika mji wa Bethlehemu, nchini Israel miaka 2000 iliyopita.

Sikukuu hii huenda sambamba na sherehe za kuaga mwaka 2021 na kuukaribisha 2022, na kila mmoja hukamilisha furaha yake kwa kadri anavyoona.

Wapo wanaosafiri kwenda vijijini kuungana na wanafamilia wengine kufurahia siku hiyo muhimu, wengine kutembelea vivutio mbalimbali nje ya nchi na kutembelea sehemu za starehe ili kusherehekea sikukuu hizo.

Kipindi hiki ndicho kumbi za starehe huandaa starehe tofauti ikiwamo muziki kwa watu wazima na watoto, lakini wengine huondoka wote nyumbani kwenda kutembea ilimradi kukamilisha furaha yao ya kusherehekea sikukuu hizo.

Ni kipindi ambacho hutumiwa na wahalifu kuzunguka nyumba za watu kufanya wizi, hivyo tahadhari lazima ianzie nyumbani, safarini na kwenye sehemu za starehe ili kuepusha majanga.

Kwa wale watakaoendesha magari binafsi, hadi sasa ajali nyingi zinaripotiwa kwenye barabara za kwenda mikoani hususani Kanda ya Kaskazini ambako watu wengi wanakwenda kuungana na familia zao vijijini.

Ni lazima kukumbuka kwenye vyombo vya usafiri wamepakiza ndugu jamaa na marafiki, lakini wanaendesha bila tahadhari ya kufuata alama za usalama barabarani kiasi cha kusababisha majanga kwa familia.

Ni muhimu dereva awe amepumzika vya kutosha, kufuata alama za barabarani, na kubwa zaidi asiendeshe gari akiwa amekesha kwenye pombe na kuamkia safari.

Wengi huondoka alfajiri kabla askari wa usalama barabarani wanaopiga picha hawajaingia barabarani na muda huo huwa kunatokea ajali nyingi, kwa sababu ya kuendesha kwa kasi ili wawahi kufika jambo ambalo ni hatari.

Pia, ni muhimu kwa familia kutambua kuwa wakati huu wahalifu hutumia mwanya huo kuzunguka kwenye nyumba ambazo wanafamilia wameondoka bila kuacha ulinzi kwa nia ya kufanya wizi.

Lazima wazazi wafuatilie watoto wao wanakokwenda kutembea kwa kuwa kipindi hiki hupotea au kujiingiza kwenye mambo mabaya kwa kukosa usimamizi wa watu wazima.


Familia nyingi huruhusu watoto kwenda kwenye fukwe mbalimbali kwa ajili ya kupata upepo na kufurahi, lakini ni muhimu watoto wawe chini ya uangalizi wa mtu mzima ili wasifanyiwe vitendo vibaya.

Wengine hufurahi kwa kunywa pombe kupita kiasi halafu wanaendesha magari jambo ambalo ni hatari linaloweza kusababisha ajali na kuumiza au kupoteza uhai wa wasiohusika.

Tunaamini Jeshi la Polisi lenye dhamana ya kulinda raia na mali zao wataimarisha ulinzi kwenye maeneo mengi, ikiwamo ya fukwe ili kuhakikisha watu wanakuwa salama na kupunguza matukio mabaya.

Ni muhimu kila mmoja akasherehekea kwa tahadhari na kuweka akiba huku wakikumbuka Januari yenye mambo mengi ikiwamo ada, kodi za nyumba na mahitaji ya watoto shule, hivyo ni lazima kufanya kila kitu kwa kiasi na kuweka akiba.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Hii shida ya umeme kukatika saa nyingi Mwanza iangaliwe



Na Anthony Gervas, Mwanza

**MAREKEBISHO** ya mfumo mzima wa uzalishaji na usambazaji wa umeme kupitia Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), inatakiwa utoaji wa huduma ya mgao wa umeme kwa wananchi kuzingatia shughuli za uzalishaji na hali halisi ya maisha yao.

Napenda kusema wahusika wanaosimamia kazi hiyo,wazingatie bila kuwa na upendeleo wa mgao pasipo kujali matajiri au umaskini wa wananchi, ambao wengi wanaendesha maisha yao kwa kufanya shughuli za uzalishaji zinazotegemea umeme.

Wapo wajasiriamali wenye viwanda vidogo waliojiajiri wenyewe kama vile wachomaji vyuma,wanaotegemea nishati hiyo ndipo wafanye kazi ya uzalishaji mali na kuendesha maisha yao ya kila siku katika familia zao.

Nimesema hivyo, kwa sababu mgao huo wakati mwingine umekaa mkao wa matege ya binadamu, unakuta baadhi ya maeneo ya wananchi huduma za umeme mchana hazipatikani kabisa mara kwa mara kuanzia asubuhi, lakini ikifika jioni au usiku ndipo umeme unaibuka na wahusika wa shughuli za uzalishaji wanakuwa wameshafunga biashara na kuondoka.

Hali hiyo ndiyo inaturudisha nyuma Watanzania wenzangu,sababu umeme unakatwa tu 'chwaa' bila ya kuzingatia mazingira yaliyopo na athari za uzalishaji zinazoweza kutokea, hivyo wataalamu wetu hususani shirika laTanesco wanatakiwa kuwa waungwana, kwanza wasikate kwa saa nyingi zaidi.

Hatukatai au kupinga hatua zilizochukuliwa na serikali kuhakikisha marekebisho ya miundombinu ya nishati inaboreka zaidi, ili kuepuka baadaye serikali kutumia gharama kubwa zitokanazo pengine na madhara yanayoweza kujitokeza zaidi katika mashine za kutoa huduma ya uzalishaji na usambazaji umeme.

Katika hilo, nampongeza Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kuliona na kulichukulia hatua mapema, kabla ya kuleta madhara zaidi. Pia, nimuombe afanye ziara rasmi kwa ajili ya kukagua mabwawa ya maji ili kujua kama hayajafanyiwa mchezo wa kutobolewa na wajanja fulani waliozoea kusingizia vina vya maji kupungua.

Serikali imelenga hapo, baadaye kuwa na umeme wa uhakika kuondoa aibu za kukatika tena umeme mara kwa mara,.

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, wewe ndiye kiranja mkuu serikalini, ikiwamo Wizara ya Nishati, hivyo liangalie jambo hili kwa macho mawili kuepuka kasoro zisizo na sababu kutokea kwa watendaji wa Tanesco, wanakata umeme muda mrefu wakisingizia mgao, kumbe vinginevyo.

Mfano nimeshuhudia zaidi ya mara tatu huku jijini Mwanza, umeme unakatika pengine mchana saa kadhaa na kurudi usiku watu wenye huduma za ofisi zinazotegemea umeme au viwanda vidogo wanakuwa wameshafunga ofisi zao na kwenda nyumbani, sasa uzalishaji wao siku hiyo unakuwa umekwama.

Waziri wa Nishati, Januari Makamba, ahakikishe anasimamia mgawo huo kwa wananchi ufanyike bila upendeleo wa matabaka ya kitajiri au maskini, tunaamini Rais wetu alikuamini na kukuteua katika nafasi hiyo akijua unaweza kuisimamia vema na kuwang'oa wanaokwenda tofauti na matakwa ya serikali.

Nimesema mabwawa hayo yakaguliwe sababu wakati wa awamu ya nne, kukatika kwa umeme lilikuwa ni jambo la kawaida, lakini baada ya kuingia madarakani awamu ya tano kuligundulika kuwepo kwa watumishi kuhusika na hujuma za kupiga dili ili kusingizia kina cha maji kupungua kwenye mabwawa husika, serikali ilichukua hatua za haraka kudhibiti uozo huo.

Kuna jambo ambalo mimi kila siku linanishangaza, kwamba wapo wanaopenda maneno ya uongo yaliyochanganywa na kachumbari, kuliko mtu anayesema ukweli, watendaji wa aina hiyo ni hatari sana katika majukumu ya kiufundi kwa wananchi.




Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa Bank Of Africa Tanzania, Wasia Mushi (wapili kulia), Meneja Masoko wa Kitengo cha Digital, Fortunatus Joachim, (kulia), Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Kidigitali wa Benki hiyo Aman, Anord (kushoto) na Meneja Masoko wa benki hiyo, Beatrice Mirigo wakionyesha kadi ya VISA Green wakati wa hafla ya uzinduzi iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wawili wauawa mapigano wakulima na wafugaji

**Na Dege Masoli,** KILINDI

WATU wawili wakulima wa Kijiji cha Kibirashi, wilayani Kilindi mkoani Tanga, wameuawa kinyama na wengine kadhaa kujeruhiwa katika mapigano baina ya wafugaji wa jamii ya Kimasai na wakulima yaliyodumu kwa siku mbili.

Vile vile, nyumba mbili za kulala wageni zinazomilikiwa na jamii ya wafugaji wa Kimasai, zinadaiwa kuharibiwa na wananchi wenye hasira huku watu kadhaa wakijeruhiwa.

Tukio hilo ambalo limethibitishwa na polisi, linadaiwa kutokea juzi majira ya saa saba mchana kwenye mashamba ya wakulima wa kijiji hicho kabla ya kuhamia kwenye makazi ya watu baada ya mifugo ya wafugaji hao kuingia katika moja ya shamba la mwananchi.

Ilielezwa kuwa baada ya mifugo hiyo kuingia shambani, wakulima waliamua kuikamata, hatua iliyopingwa na wachungaji na kuamua kuwatoa kwa nguvu mikononi mwa wakulima.

Athuman Idd, miongoni mwa mashuhuda hao aliiambia Nipashe kuwa wakati wakiendelea na shughuli zao za kilimo, walisikia kelele ya kuomba msaada na walipokwenda walimkuta mtu mmoja akiwa amejeruhiwa kwa

mkuki maeneo mbalimbali ya mwili wake.

"Tuliamua kumkimbiza hospitali lakini cha kushangaza wafugaji hao waliendeleza mashambulizi dhidi ya watu wengine na jana ambayo ni siku ya pili walimshambulia na kumuua mwenzetu mmoja," alidai Idd.

Said Ramadhan, alivilaumu vyombo vya ulinzi na usalama, akidai ndiyo vyanzo vya mauaji na uharibifu wa mali unaotokea mara kwa mara kwa kutochukua hatua za kukomesha tabia hiyo.

"Haya ni mauaji ambayo tumeyazoea sasa ni zaidi ya watu watano wameuawa na Wamasai na hakuna hatua zozote zinazochukuliwa na wenzetu wanatamba kwamba wana hela hivyo wataendelea kutuua," alisema Ramadhan.

Diwani wa Kata ya Kibirashi, Bakari Fau, alikiri kutokea mauaji hayo na kumtaja mmoja, Mbelwa Mhamba, kuuawa katika mgogoro huo akiwamo mwingine wa jamii ya wafugaji ambaye hata hivyo hajafahamika jina na wengine wakijeruhiwa.

Fau aliiomba serikali kuingilia kati mgogoro huo ambao umekuwa tishio kwa maisha ya watu na mali zao kwa kuwa mauaji hayo yamekuwa yakitokea kila mara.

Alisema pia watu wasiojulikana walivamia nyumba mbili za kulala wageni zinazomilikiwa na jamii ya Wamasai kijijini hapo na kufanya uharibifu mkubwa kwenye nyumba hizo.

Hata hivyo, alipopigiwa simu Mkuu wa Wilaya ya Kilindi, Abel Busalama, kuhusu tukio hilo, alituma ujumbe mfupi kuwa yupo kwenye mkutano kijiji cha Kibirashi na baadaye kijiji cha Mafisa kwa ajili ya suala hilo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Sofia Jongo, aliahidi kuzungumza na waandishi wa habari kwa kuwa muda aliopigiwa alikuwa kwenye kikao cha operesheni maalumu.

## Wafugaji watakiwa kusajili mifugo

**Na Mwandishi Wetu**

WAFUGAJI wamepewa muda hadi Agosti mwakani kushiriki usajili, utambuzi na ufuatiliaji wa mifugo kwa kuweka alama za kielektroniki.

Watakaoshindwa kufanikisha, hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

Mkurugenzi Msaidizi Huduma za Ukaguzi Wanyama kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Annette Kitambi, alisema hayo mkoani Morogoro wakati wa uzinduzi huo unaolenga kuondoa migogoro ya wakulima na wafugaji ambayo ni kero nchini.

"Baada ya mwezi wa nane mwakani mfugaji hataweza kuuza au kwenda kuchinja mfugo ambao haujawekwa alama," alisema Dk. Kitambi.

"Hiyo yenyewe ni motisha ya kumlazimisha mfugaji afanye utambuzi kwa sababu ng'ombe na punda ni Sh. 1,750 na hii inafanyika mara moja na hereni ile haichomoki kwa sababu ina ubora safi," alisema.

Kaimu Katibu Tawala wa mkoa huo, Injinia Hezron Kilamhama, alisema mkakati huo licha ya kuondoa migogoro hiyo, utasaidia katika ukuzaji wa biashara kwa wafugaji.

"Pia, zoezi hili ni hakikisho la soko la kimataifa kwa mujibu wa sheria zilizowekwa na sasa wameweka shinikizo la alama za utambuzi kwa ajili ya mifugo kuuzwa nje ya nchi," alisema Injinia Kilamhama.

Serikali imebuni njia hiyo mpya ya utambuzi mifugo kwa ajili ya upatikanaji wa takwimu sahihi za mifugo baada ya upigaji chapa iliyozinduliwa mwaka 2017 kukumbwa na matatizo mengi ambayo yalifanya kutokuwa na ufanisi.

# Lukuvi apongeza kasi upimaji mpaka Tanzania na Kenya

**Na Munir Shemweta,** TARIME

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, juzi alikagua uimarishaji mpaka wa kimataifa kati ya Tanzania na Kenya katika eneo la Hifadhi ya Taifa ya Serengeti mkoani Mara na kupongeza wapimaji kwa kufanikisha kuweka alama 205.

Pia Waziri Lukuvi aliwashukuru marais wa Tanzania na Kenya kwa kukubaliana kuendelea na uimarishaji mpaka huo wa kimataifa kwenye eneo la Hifadhi za Taifa za Serengeti na Masai Mara kwa upande wa Kenya ambapo uimarishaji wake ulisimama kwa muda.

"Kwa muda mfupi timu za nchi hizo mbili zimeweka alama 205 katika eneo hili. Kazi ilianza 2018 tulipofika eneo la hifadhi tulisimama kidogo na uendelezaji huu unaofanyika umechangiwa na ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan kule nchini Kenya kuzungumza na mwenzake Uhuru Kenyatta na kukubaliana ndiyo maana wapimaji wamendelea na kazi hii," alisema Lukuvi.

Akiwa katika eneo la Serengeti wakati wa ziara ya kukagua uimarishaji mpaka wa kimataifa kati ya Tanzania na Kenya, Waziri Lukuvi alisema anaamini nchi hizo zitamaliza kuweka alama kwenye mpaka mzima unaofikia kilomita 758 ambapo kwa sasa zimefikiwa kilomita 232 na kuahidi zote kumalizwa.

Akigeukia kuhusu eneo la ukingo wa mpaka (Buffer Zone), Lukuvi alisema kwa sasa ni vyema utengenezaji barabara ukazingatia eneo la mita tano aliyoieleza kuwa ni mwafaka wa nchi hizo mbili na kuongeza kuwa mazungumzo bado yanaendelea kuona kama kuna haja ya eneo hilo kuongezwa.

"Serikali itaendelea kusaidia ili kazi hii ya uimarishaji mipaka ya kimataifa iende vizuri na uwekaji alama hizi si uadui bali ni kuwa na mipaka inayoonekana itakayoondoa hofu. Mtu akitaka kufanya uovu asisingizie kama hajui mpaka na alama tutaweka kote hata majini," alisema. Mkurugenzi wa Upimaji Ramani wa Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Hamdouny Mansour, alisema kazi mbalimbali zimefanyika wakati wa uimarishaji mpaka huo zikiwamo utoaji elimu, kuainisha sehemu za kujenga alama za mpaka pamoja na kukusanya taarifa za kijiografia.

Mpimaji kutoka Idara ya Upimaji nchini Kenya, Ibrayan Sabwa, alisema katika kipindi chote cha kazi ya uimarishaji mpaka eneo la Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na ile ya Masai Mara kwa upande wa Kenya wamekuwa na ushirikiano mzuri na kubainisha kuwa hakukuwa na shida yoyote wakati wa kazi hiyo.

"Tumekuwa tukiendelea vizuri, na kazi imeenda vizuri sana, Watanzania wamekuwa wakishirikiana na sisi vizuri hawakuwa na shida yoyote na nina imani kazi itakamilika vizuri. Watanzania ni marafiki zetu na wao ni marafiki zetu," alisema Sabwa.

Mpango kazi wa mwaka wa fedha 2021/22 kuhusiana na uimarishaji mipaka wa Tanzania na Kenya ni kukamilisha awamu ya kwanza ya kilometa 238 kwa kukamilisha kipande cha hifadhi cha eneo la Natron la kilometa 23 pamoja na kuimarisha awamu ya pili yenye kilomita 110 ya mpaka kutoka Ziwa Natron hadi Namanga katika Wilaya ya Longido.

Mpaka wa Tanzania na Kenya una urefu wa nchi kavu wa kilometa 758 uliowekwa kwa makubaliano ya wakoloni wa Kijerumani na Kiingereza mwaka 1893 chini ya mkataba wa Anglo-Germany Agreement na itifaki yake kukubalika mwaka 1906.

## LG yafungua duka la kisasa zaidi Dar

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya vifaa vya kielektroniki ya LG, imefungua duka lake la tatu jijini Dar es Salaam kwa kushirikiana na mshirika wake, Garnet Star, kwa lengo la kuwapa wateja nafasi ya kupata uzoefu wa aina yake wa teknolojia mpya.

Garnet Star Ltd ni kampuni iliyoanzishwa miaka minane iliyopita na ni wakala aliyethibitishwa na kuidhinishwa kuuza bidhaa za LG na kufanya matengenezo kwa upande wa Tanzania.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa duka hilo juzi, Mkurugenzi Mtendaji wa LG Electronics Afrika Mashariki, SaNyoung Kim, alisema hilo ni duka la tatu na kubwa kushinda yote baada ya uzinduzi wa maduka mawili Juni, mwaka huu, katika juhudi za kujitanua zaidi nchini Tanzania.

Kwa mujibu wa Kim, LG Electronics imepata mafanikio makubwa na endelevu katika nyanja zote za bidhaa zake ikiwemo bidhaa aina ya B2C na B2B na pia katika hadhi ya Premium kama vile OLED TV, friji za InstaView, microwave aina ya Neochef na mashine za kufua nguo aina ya TWINWash& Vivace huku akisema wateja wametokea kupenda bidhaa hizo zaidi. Alisema wanatarajia kuona bidhaa zenye hadhi ya premium zikiuza zaidi.

"Jiji la Dar es Salaam limekaa vizuri kwa sababu lina wateja wengi. Baada ya kufungua maduka mawili, tuliendelea kupata wateja wengi zaidi hadi tukaamua kuongeza duka lingine. Tunaahidi kuendelea kuwapa wateja wetu uzoefu wa aina yake katika manunuzi yao ambapo pia wanaweza kupata huduma ya matengenezo na maelekezo kutoka kwa wataalamu wetu waliobobea," alisema.

"Katika miezi ijayo, tutafungua maduka mengine na kufanya maduka mengine 12 yaliyoko Afrika Mashariki yawe ya kisasa zaidi ili kukidhi matakwa ya wateja wetu ambao wanaongezeka kila siku na kuwapa uzoefu wa aina yake wa teknolojia mpya na bidhaa za LG," alisema Kim.

Alisema wateja wengi wamekuwa wakinunua bidhaa za umeme za nyumbani zikiwamo za kiteknolojia, za kielimu, mapishi, burudani na urembo.

"Ni wazi kuwa wakati huu wa janga la corona, wateja wengi wameigeukia teknolojia pamoja na uvumbuzi ambao unasababisha ufanisi na afya bora," alisema Kim.

LG kwa sasa inazalisha bidhaa nyingi zenye hadhi ya Premium katika eneo la Afrika Mashariki zenye lengo la kusaidia watumiaji kuhifadhi nishati na maji, hivyo kuwa rafiki kwa mazingira katika hali ya kuunga mkono Malengo Endelevu ya Maendeleo.

# Serikali yaombwa kuokoa wanyama kutoweka

**Na Ashton Balaigwa,**
MANYARA

SERIKALI kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii imeombwa, kuokoa wanyamapori ambao wako hatarini kutoweka katika hifadhi za taifa za Tarangire na Manyara kutokana na kuathiriwa na shughuli za kibinadamu.

Hatua hiyo imesababisha kukosekana kwa mipaka ya maeneo ya mapito ya wanyama, maarufu kama Shoroba.

Ili kuokoa wanyama hao, serikali imeshauriwa kuainisha mipaka hiyo ya shoroba na kuipa nguvu za kisheria pamoja na kutoa elimu kwa wananchi ambao wanaishi pembezoni mwa shoroba hizo kubadili tabia na kufanya shughuli zao bila kuathiri shoroba.

Mhadhiri Mwandamizi kutoka Idara ya Usimamizi wa Wanyamapori ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Dk. Alfan Rija, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari kwenye mafunzo yaliyoandaliwa na Mtandao wa Ufuatiliaji wa Biashara Viumbepori Halali na Haramu katika Nchi za Afrika Mashariki (TRAFFIC).

Mafunzo hayo yanatolewa na TRAFFIC kwa kushirikina na Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET) kwa ufadhili wa Watu wa Marekani chini ya mradi unaofahamika kama CONNECT.

Dk. Rija alisema licha ya kuwapo kwa maeneo ya shoroba za wanyama, kwa sasa mengi yameharibiwa kutokana na kuvamiwa na shughuli za mifugo, kilimo na maeneo ya makazi, hivyo kusababisha kukosekana kwa chakula cha wanyamapori.

"Shoroba nyingi zimekaliwa na wananachi kwa sababu ziko katika ardhi za wananchi. Sasa shughuli nyingi za kibinadamu zinafanyika, kinachotakiwa kuzitambua na kuzipa nguvu za kisheria kama maeneo mahsusi ya kiuhifadhi ili tusiathiri wanyamapori," alisema Dk. Rija.

Alisema uvamizi huo katika maeneo ya shoroba, umesababisha athari zingine ikiwa ni pamoja na kubadilisha ikolojia, kukata miti na kuleta mabadiliko ya tabianchi. Aliishauri serikali kusimamia maeneo yaliyohifadhiwa ambayo yanaleta faida kwa taifa ikiwamo fedha zinazotokana na wanyamapori.

Ofisa Wanyamapori wa Halmashauri ya wilaya ya Babati, Christopher Laizer, alisema historia ya uhai wa hifadhi za taifa za Tarangire na Manyara inatokana na shoroba ya Kwakuchinja inayopita katika Jumuiya ya Hifadhi ya Burunge ambayo awali ilikuwa na mapito mengi ya wanyama lakini kutokana na uvamizi, imebakiwa na mapito matatu ya wanyama.

Alisema wanafanya juhudi ili kulinda shoroba hiyo kama hifadhi, lakini licha ya kutolewa kwa kanuni zinazolinda hizo shoroba ya mwaka 2018, bado haina makali ya kisheria ya kudhibiti zaidi masuala ya shughuli zenye madhara na hifadhi zikiwamo kilimo na makazi.

Awali, Mwakilishi kutoka TRAFFIC, Jane Shuma, alisema mtandao huo uko Kenya, Uganda na makao yake makuu ni Tanzania na mafunzo hayo yamelenga kuwajengea uwezo waandishi wa habari kuandika kwa usahihi na ufasaha juu ya umuhimu wa watu kuishi na viumbepori na kubadili tabia itakayosaidia kutokuleta madhara kwa viumbe.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa JET, John Chikomo, alisema mafunzo hayo ni mwendelezo wa yaliyofanywa na JET kuhusu uhifadhi wa maliasili, migogoro ya mwingiliano wa binadamu na wanyamapori katika shoroba.

Chikomo alisema lengo la mafunzo hayo ni kuongeza uelewa kwa waandishi wa habari ili kutumia taaluma yao kuhabarisha wananchi.



Baadhi ya wahudhuriaji wa tamasha la Christmas Carols 2021 wakizungusha gurudumu la bahati ili kujishindia zawadi kutoka kampuni ya Coca-Cola ikiwa ni sehemu ya kampeni ya 'Maajabu Halisi' inayoendelea nchini kote. Tamasha hilo lililoandaliwa na Clouds Media Group kwa kushirikiana na Coca-Cola Tanzania ambapo wasanii mbalimbali wa muziki wa injili walitumbuiza katika viwanja vya Mlimani City jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki hii.

# NMB yashinda tuzo ya benki salama zaidi nchini

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imeshinda tuzo ya ubora wa benki salama zaidi nchini kwa miaka miwili mfululizo iliyotolewa na jarida la Global Finance la New York Marekani.

Aidha, benki hiyo imewahi kushinda tuzo nyingine ya wa utayari wa NMB kulihudumia taifa, uimara wake kifedha na kuendelea kuongoza sokoni.

Akitangaza mafanikio hayo, Ofisa Mkuu wa Fedha wa NMB, Juma Kimori, alisema jarida hilo limewapa heshima hiyo kutokana na kuibuka kinara katika vigezo kadhaa vya kifedha, ikiwa ni pamoja na uimara wa mtaji na ukubwa wa mali za benki.

"NMB imetajwa kuwa benki salama zaidi Tanzania 2021 baada ya kuangalia vigezo kadhaa ikiwa ni pamoja na ufanisi na utendaji kwa ujumla, mkakati wa huduma za kidijitali, huduma jumuishi za kifedha na usalama wa huduma za kimtandao," alisema Kimori na kuongeza;

"Sababu zingine zilizotufanya kupata tuzo hii ni mapato yatokanayo na mali za benki, kiwango cha amana za wateja, kiwango cha mikopo pamoja na uwiano wa mikopo na amana za wateja. Na katika vigezo vyote hivyo, tumekuwa vinara kwa hapa Tanzania," alibainisha.

"Kuaminika na kutambulika huku na taasisi kubwa ulimwenguni kama Global Finance kwa mara mbili mfululizo ni fahari kubwa kwetu, lakini inatuachia changamoto ya kuendelea kujituma katika kuhudumia na kubuni suluhisho zitakazo tufanya tubaki kuwa vinara katika huduma za kifedha hapa nchini," alisisitiza.

Tuzo za benki salama zaidi duniani hufanyika kila mwaka kwa mabara yote na kwa kila nchi na hutolewa baada ya kufanyika tathmini ya vigezo vya kifedha na kiutendaji.

Kwa mujibu wa Kimori, ushindi wa NMB unathibitisha uimara na uthabiti wa taasisi hiyo pamoja na mabadiliko ya kidijitali inayoyafanya na uwezo wake kiubunifu katika kuwasaidia wafanyakazi, wateja na jamii kwa ujumla.

Hii ni tuzo ya saba ya kimataifa kunyakuliwa na NMB mwaka huu na kufanya jumla ya tuzo ilizoshinda kuwa nane.

# Wairani washerehekea usiku mrefu zaidi

**Na Kulwa Mzee**

MKURUGENZI wa Kituo cha Utamaduni cha Irani nchini, Morteza Perani, amewaomba wananchi kushirikiana na Wairani kusherehekea usiku wa Chelleh ambao hufanyika wakati huu usiku unapokuwa mrefu zaidi na kufuatia mchana kuwa mrefu katika nusu ya kaskazini mwa dunia.

Akizungumzia sherehe hiyo ofisini kwake jijini Dar es Salaam jana, alisema hufanyika usiku wa leo ambao kwa kawaida, familia za Kiirani huandaa na kula chakula kizuri cha usiku pamoja na matunda na hasa tikitimaji na komamanga.

Alisema, wanafamilia hula vitafunwa tofauti, hutoa visa mbalimbali na kisha wakubwa wa familia huwasomea wanafamilia baadhi ya beti za mashairi za malenga Hafez.

"Kwa maelfu ya miaka sasa, Wairani wamekuwa wakisherehekea usiku huo wa mwisho kwa kutekeleza mila na desturi katika miji mbalimbali nchini Iran, usiku unaotajwa kuwa ni mrefu zaidi wa mwaka na wenye giza nene.

"Historia inaeleza kuwa, sherehe ya usiku wa Chelleh ilianza zama za kale na wala haifahamiki ni muda gani hasa ilipoanza, lakini wanasaikolojia walio wengi wanaeleza kuwa, usiku huo ulianza yapata miaka elfu saba iliyopita," alisema.

Alisema usiku huo ulitambuliwa rasmi miaka 500 kabla ya kuzaliwa Kristo na historia yake kuingizwa kwenye kalenda rasmi ya Wairani wa kale katika zama za Daryush wa kwanza, ambayo inajumuisha kalenda za Wamisri na Wababeli.

Akifafanua alisema, Wairan wa zamani waliugawanya msimu wa baridi kuwa "Chelleh Kubwa" na "Chelleh Ndogo", ambao ulikuwa na sehemu mbili za siku arobaini.

Alisema baada ya siku arobaini hufanyika sherehe ya kumalizika Chelleh kubwa na kuanza Chelleh ndogo.

"Kwa mujibu wa mila na desturi za kale za usiku huo ufikapo wafalme wa Kiirani waliweka chini mataji yao ya kifalme, huelekea jangwani wakiwa wamevalia nguo nyeupe na kukaa juu ya mazulia meupe.

"Watu wote kwenye kasri ya mfalme, wahudumu na watumwa hupewa uhuru wa kwenda mjini na kuishi kama watu wengine na watu wote iwe mfalme, waziri au watu wa kawaida huwa sawa na wenye kulingana," alisema.

# Akutwa juu ya mti akiwa amelala fofofo

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

UKISTAAJABU ya Musa utayaona ya firauni, ndivyo ilivyotokea kwa mkazi wa mkoani Mbeya, Saili Juma (27), aliyejikuta wilayani Masasi, mkoani Mtwara akiwa amelala juu ya mti fofofo katika Mtaa wa Misufini, Kata ya Migongo.

Tukio hilo lililostaajabisha na kuacha gumzo kwa wananchi wilayani Masasi, limehusishwa na imani za kishirikina.

Akizungumza na Nipashe jana, katika wodi namba moja Hospitali ya Halmashauri ya Masasi Mkomaindo, kijana huyo alisema hafahamu amefikaje wilayani Masasi ilhali alikuwa nyumbani kwao Mbeya akiwa na bibi yake ambaye anaishi naye.

Alisema anachofahamu ni kwamba juzi usiku akiwa kwao alifanya shughuli zake za kila siku kama kawaida akiwa nyumbani kwao Mbeya na muda wa kulala aliingia chumbani kwake, lakini ameshangaa kujikuta akiwa wilayani Masasi bila kujitambua juu ya mti amelala fofofo.

Juma alisema alipoingia chumbani kwake kulala siku hiyo ya Jumapili mkoani Mbeya, ameshangaa kujikuta wilayani Masasi, jambo linalomshangaza na kujiuliza maswali amefikaje wakati alikuwa Mbeya nyumbani kwao.

"Mimi ni mkazi wa Mbeya ndiko nyumbani kwetu na ninaishi na bibi yangu na mpaka jana usiku nimerudi kazini kwangu ninakouza CD za filamu na muziki na tumekula chakula pamoja na bibi, ila nashangaa saa hizi kujiona niko hapa wilayani Masasi nimefikaje ni swali ambalo hata mimi mwenyewe najiuliza," alisema Juma kwa mshangao.

Wakizungumza na gazeti hili kuhusu tukio hilo, baadhi ya mashuhuda waishio Misufini Migongo, wilayani Masasi walisema, walimgundua kijana huyo akiwa amelala juu ya mti majira ya saa 2:00 usiku licha ya taarifa zake za kuwapo juu ya mti huo kuanza kusambaa majira ya saa mbili asubuhi.

Ahmadi Ally, mkazi wa Migongo alisema, baada ya kufika katika mti huo na kushuhudia tukio hilo, walifanya jitihada za kumshusha chini kwa kushirikiana na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, wilayani Masasi. Alisema alipoteremshwa alikuwa katika usingizi mzito wa kutojitambua na wananchi hao walimwagia ndoo kadhaa za maji, lakini hakuzinduka usingizini.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Serikali wa Mtaa huo, Jojina Milanzi, alisema uongozi wa mtaa baada ya kushuhudia tukio la kijana huyo akiwa juu ya mti, walipiga simu kituo cha polisi ili waje kumteremsha.

Akithibitisha tukio hilo Kaimu Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Wilaya ya Masasi, Bakari Nirabu, alisema walipomshusha chini alikuwa hajitambui licha ya kumwagiwa maji baridi kama kumpatia huduma ya kwanza, hata hivyo hakuweza kuzinduka.

"Tulipigiwa simu na Jeshi la Polisi kuhusu kijana huyo na tulifika sehemu ya tukio tulimkuta kijana huyo akiwa amelala juu ya mti, tulimshusha chini na baadaye tulimkimbiza Hospitali ya Mkomaindo, lakini leo (juzi) asubuhi tumeshangaa tulipoambiwa na wahuduma wa hospitali hiyo kuwa kijana huyo ni mkazi wa Songwe na hajui amefikaje wilayani Masasi," alisema Kamanda Nirabu.




Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ng'wilabuzu Ndwata Ludigija, akifurahia na mshindi wa Sh. milioni 10 wa Biko, Mikidadi Kaimu Ngoo, alipomtembelea ofisini kwake kumkabidhi hundi yake ya ushindi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kigoma yazindua mpango kazi kukomesha ukatili wa kijinsia

**Na Mwandishi Wetu,** KIGOMA

MKOA wa Kigoma umezindua mpango kazi kuhakikisha vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto vinatokomezwa na kuondoa nafasi ya mkoa huo kuwa miongoni mwa inayoongoza kwa vitendo hivyo.

Akizindua mpango kazi huo, Katibu Tawala Mkoa wa Kigoma, Rashid Mchatta, alisema atasimamia halmashauri zinatenga bajeti kutekeleza mkakati huo kwa kuwa ni wajibu wa kila mmoja kuweka juhudi na jamii kuwa na uelewa kuhusu madhara ya vitendo hivyo.

"Yote ambayo yameazimiwa katika mpango huu yatatekelezwa na kuhakikisha sheria inachukua mkondo wake kutokomeza vitendo hivyo. Ni lazima kila mmoja kwa nafasi yake awajibike baada ya kutoka hapa na tutakuwa tumewatendea haki wanawake na watoto. Suala la lishe na hili la ukatili wa watoto na wanawake tutayatilia mkazo," alisema Mchatta.

Akizungumza kabla ya uzinduzi huo, Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Jinsia kutoka Wizara ya Afya, Mwajuma Magwiza, alisema mpango kazi huo utaendeleza kwa kasi kampeni ya 'Twende Pamoja Ukatili Sasa Basi', ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA).

"Suala hili siyo la kuiachia serikali ila wanajamii na wadau sote kwa pamoja tuungane mkono juhudi hizi kwa ajili ya kuweka bajeti zetu ambazo zote zitaelekeza nguvu katika kupambana na ukatili uliopo mkoani Kigoma na Tanzania nzima," alisema Magwiza.

Aidha, Magwiza amehimiza jamii ishirikishwe katika utekelezaji wa mpango huo na kupata taarifa katika kila hatua inayofikiwa.

Akiwasilisha mpango kazi huo, Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Maendeleo ya Jinsia, Grace Mwangwa, ameikumbusha jamii kutekeleza wajibu wao kulingana na nafasi zao na kwamba mpango huo umejumuisha masuala mbalimbali yaliyoainishwa na wadau katika kongamano lililofanyika awali.

Grace alisisitiza wananchi kutoa taarifa za vitendo vya ukatili kwa watoto na wanawake kwenye mamlaka ili hatua zichukuliwe kwa wanaofanya vitendo hivyo.

"Ukatili mwingi unaanzia ndani ya familia kwa sababu vitendo vinapotokea wanaamua kuyamaliza nyumbani hali inayosababisha ukatili kuongezeka kwani wanaofanya vitendo hivyo wanakuwa hawajachukuliwa hatua," alisema Grace.

Kwa upande wake mmoja wa viongozi wa dini aliyeshiriki katika uzinduzi huo, Shekhe Rashid Haruna Hamis, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya MTAKUWWA katika Kata ya Gungu, Kigoma Ujiji, alisema kuwa serikali inafanya vyema kushirikiana na wadau wote kukemea vitendo vya ukatili, akitaja mmomonyoko wa maadili ni chanzo kikubwa kusababisha vitendo hivyo.

Baadhi ya wananchi na wadau walioshiriki kuandaa mpango kazi huo baada ya majadiliano ya kina, akiwamo Beatrice Mtesigwa na Gervas Lwako, walisema mitandao ya kijamii ni changamoto kwa kizazi cha sasa na kuomba mamlaka zinazohusika kuhakikisha kesi za vitendo hivyo zinafanyiwa kazi haraka.

Mpango kazi huo umeandaliwa kwa pamoja na wadau mbalimbali wa mkoa huo walioshiriki kongamano la siku mbili lililoandaliwa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kupitia Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii kwa lengo la kujadili namna ya kutokomeza vitendo vya ukatili mkoani hapo na kukubaliana kaulimbiu ya mpango huo ni Twende Pamoja, Ukatili Kigoma sasa basi.

# 'Wanaojifungua mapacha wasaidiwe kumudu maisha'

**Na Sabato Kasika**

JAMII imetakiwa kuibua familia zenye watoto mapacha zinazokabiliwa na ugumu wa maisha ili zisaidiwe kwa hali na mali ziweze kumudu gharama za kuwahudumia watoto hao.

Wito huo ulitolewa jijini Dar es Salaam jana na Mwenyekiti wa shirika linalosaidia wazazi wenye mapacha walio na maisha magumu la Eden Twins Foundation, Diana Joy Mbena, jijini Dar es Salaam juzi.

Mwenyekiti huyo alikuwa katika Mtaa wa Buguruni Mivinjeni kwa ajili ya kutoa msaada wa vitu mbalimbali ukiwamo unga wa dona, sukari na sabuni kwa Grace Ngoje, aliyejifungua mapacha watatu.

Alisema, katika jamii wapo wazazi wenye watoto mapacha wanaokabiliwa na ugumu wa maisha akiwamo huyo aliyepewa msaada ambaye aliibuliwa na serikali ya Mtaa wa Buguruni Mivinjeni.

"Jamii iendelee kuibua familia kama hizi na ikiwezekana ishiriki pia kuzisaidia kwa hali na mali familia hizo ili kuzipunguzia makali ya maisha kwa kuwa kulea watoto wawili au watatu bila msaada ni kazi ngumu," alisema Diana.

Alitoa mfano wa maisha ya Grace kwamba ni magumu, anakula kwa shida kutokana na ukosefu wa fedha za kununua mahitaji ya kila siku.

"Mimi Mwenyekiti wa Eden Twins Foundation, tulipata taarifa za ugumu wa maisha unaomkabili mzazi huyu, nami kwa kushirikiana na wadau wengine tumekuja kumsaidia kidogo tulichonacho," alisema.

Alisema, Eden Twins Foundation bado ni shirika changa na limekuwa likijitahidi kuwazungukia wazazi wenye watoto mapacha na kuwasaidia kwa hali na mali kadiri inavyowezekana.

Grace kwa upande wake alisema, aliyempa mimba alimkimbia wakati ana ujauzito wa miezi mitatu, na kwamba anahangaika mwenyewe kuwalea watoto wake ambao kwa sasa wana umri wa mwezi mmoja.

"Nina maisha magumu, wakati mwingine wanapolia sana huwa ninatamani kukimbia wabaki peke yao, lakini ninasita. Ninashukuru kwa msaada wenu na mmenitia moyo niendelee kuvumilia," alisema Grace.

Aidha, alisema, huwa anafanya biashara ya kuuza mboga katika soko la Ilala ambayo haimwingizii kiasi kikubwa cha fedha, hali inayosababisha ashindwe kumudu gharama za maisha hasa wakati huu anaolea mapacha watatu.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Buguruni Mivinjeni, Fadiga Legele, alisema, mzazi huyo anaishi maisha magumu na kwamba ofisi yake imekuwa ikijitahidi kuhamasisha wadau mbalimbali kumsaidia.

"Tulishaita waandishi wa habari wakaja kwa ajili ya kumhoji ili kutoa taarifa zake umma wa Watanzania ujue na kuangalia jinsi ya kumsaidia na sasa wamekuja Eden Twins Foundation," alisema Legele.

Legele alisema, katika mtaa wake, ana taarifa za mzazi huyo tu ambaye anakabiliwa na ugumu wa maisha, na kufafanua kuwa inawezekana wakawapo wengine ambao taarifa zao hazijafika ofisini kwake.



Mwenyekiti wa Shirika lisilo la Kiserikali la Eden Twins Foundation, Diana Joy Mbena (kulia), akimkabidhi Grace Ngoje, ndoo ya sabuni ambayo ni sehemu ya msaada ulitolewa na shirika hilo kwake, ili kukabiliana na ugumu wa maisha, Buguruni Malapa jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Vikundi vyaagizwa kurejesha mikopo kwa wakati

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

KATIBU Tawala wa Wilaya ya Kibaha, Sozi Ngate, ameviagiza vikundi vya wajasiriamali vinavyonufaika na mikopo ya halmashauri kurejesha kwa wakati ili kutoa fursa kwa wengine kupata.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, Sara Msafiri, jana mjini Mlandizi katika hafla ya kutoa mikopo kwa wajasiriamali, aliwataka kuondoa dhana waliyojijengea baadhi yao kwamba kurejesha mikopo hiyo si lazima.

Ngate alisema baadhi ya vikundi vimekuwa vikichukua fedha hizo na kushindwa kurejesha kwa wakati jambo ambalo linakwamisha wengine kunufaika.

"Sambamba na utaratibu mzuri unaofanywa na halmashauri kuhakikisha fedha hizi zinatengwa na kutolewa kama kanuni inavyoelekezwa, kikwazo kipo kwenye urejeshaji mbaya wa baadhi ya vikundi, naagiza vikundi vilivyopo hapa leo muondoe dhana hii," alisisitiza.

Alitoa wito kwa vijana kujishughulisha na ujasiriamali na kuomba mikopo kwa kuwa kwasasa inaonekana uwiano usio sawa kati ya vikundi vya wanawake na vijana.

"Sababu inayoelezwa kuchangia uwiano usio sawa kwenye utoaji wa mikopo ni vijana wengi kutopenda kufanya kazi za pamoja na kuwa wazito kujiunga katika vikundi hivyo kukosa vigezo, nawasihi vijana kutumia fursa hii muweze kunufaika na mikopo na mjikwamue kiuchumi," alisema.

Akitoa taarifa ya hali ya utoaji wa mikopo kwa niaba ya Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Wilaya, Pudenciana Domel, alisema kwa mwaka wa fedha 2021/2022 halmashauri ilikadiria kukusanya Sh. bilioni 1.2 na kutenga Sh. milioni 121.3 kama asilimia 10.

Alisema kwa kipindi cha Julai hadi Desemba, halmashauri inatoa Sh. milioni 140 ambazo wanufaika walikabidhiwa hundi yenye thamani ya fedha hizo.

Pudenciana alieleza kuwa kati ya fedha hizo Sh. milioni 51.4 ni fedha kutoka mapato ya ndani ya halmashauri, Sh. milioni 63.5 ni fedha za marejesho na Sh. milioni 25 ni fedha za bakaa.

Alibainisha kuwa kati ya fedha hizo za mikopo Sh. milioni 140, zilizotolewa kwa vikundi 18 vya wanawake ni Sh. milioni 94, Sh. milioni 30.5 zinatolewa kwa vikundi vitano vya vijana na Sh. milioni 15.3 kwa vikundi vitano vya watu wenye ulemavu. Alisema pia kikwazo cha masoko ya bidhaa kwa wajasiriamali, masharti nafuu kwa urejeshaji wa mikopo na kusababisha uzorotaji wa marejesho pamoja na dhana ya vikundi kuchukuliwa mikopo hiyo kama misaada.

Awali, akimkaribisha Katibu Tawala, Kaimu Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Shukuru Lusanjala, aliwataka wajasiriamali kutumia mikopo hiyo kama mbegu na kurejesha kwa wakati.

# Wajawazito wadai kutozwa 400,000 upasuaji

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAJAWAZITO Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wamelalamikia kitendo cha kutozwa Sh.300,000 hadi 400,000 na madaktari na watoa huduma wa Kituo cha Afya Bulungwa wanapokwenda kupata huduma za upasuaji na kuiomba serikali kuingilia kati suala hilo.

Malalamiko hayo yamebainishwa jana katika mkutano wa hadhara ulioitishwa na Mbunge wa Jimbo la Ushetu, Emmanuel Cherehani, uliofanyika katika kijiji cha Mseki, Kata ya Bulungwa uliokuwa na lengo la kusikiliza kero mbalimbali zinazowakabili wananchi wa jimbo hilo.

Mmoja wa wakazi wa Kijiji cha Mseki, Mabula Shija, alisema, wajawazito wanatozwa gharama kubwa za upasuaji wanapofika katika Kituo cha Afya Bulungwa kupata huduma huku wasiokuwa na uwezo wanalazimika kujifungulia majumbani hali inayotishia vifo vya wajawazito na watoto.

"Tunaomba serikali iingilie kati suala hili na kumwondoa mganga mfawidhi wa kituo hiki kwa kushindwa kudhibiti hali hii na kusababisha wajawazito kuacha kwenda katika kituo hicho kutokana na gharama kubwa za upasuaji na kujifungulia majumbani," alisema Bundala.

Naye Dorice John, Mkazi wa Kijiji cha Nyamkondo alisema, huduma za uzazi kwa wajawazito ni shida kutokana na kulazimika kununua vifaa tiba kwa ajili ya kujifungulia licha ya kutoa fedha za upasuaji na kusababisha wengi kuanza kukimbilia kwa waganga wa jadi kupata huduma hiyo.

Pia wanaambiwa kwenda kununua dawa kwenye maduka yaliyopo nje ya kituo cha afya jambo linalowakwaza kwa kuwa dawa katika maduka hayo zinauzwa gharama kubwa ikilinganishwa na zinazitolewa kituoni.

Akijibu malalamiko hayo, Kaimu Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Ushetu, Dk. Alphonce Malunde, alisema, malalamiko hayo ndio anayasikia leo na atalifanyia kazi suala hilo kwa haraka ili kuwaondolea adha wajawazito na wananchi wanaofika katika kituo hicho.

Hata hivyo, alisema gharama za upasuaji ni Sh.100,000 kwa upasuaji mkubwa na zimebandikwa katika mbao za matangazo kwa kila zahanati na vituo vya afya vyote na kwa watoa huduma watakaobainika baada ya uchunguzi, watachukuliwa hatua za kisheria kwa kujihusisha na vitendo vya unyanyasaji wagonjwa.

Kwa upande wake, mbunge wa jimbo hilo, Emmanuel Cherehani, alisikitishwa na vitendo hivyo na kuwataka watumishi wa kituo hicho cha afya kutojihusisha na vitendo vya rushwa na badala yake wafanye kazi kwa weledi kuzingatia maadili ya kazi yao.

"Ni lazima kila mtumishi wa afya afanye biashara ya dawa? Serikali inahamasisha wananchi wawe na bima wakienda hospitali wanaambiwa dawa hakuna, lakini kwenye maduka yao zipo...nimetembelea stoo za dawa zahanati na vituo vya afya vyote jimbo hili dawa zipo za kutosha," alisema Cherehani.

Aidha, Cherehani alisema kuwa, asilimia 80 ya maduka ya dawa vijijini na mali ya watumishi wa vituo vya afya na zahanati yamegeuka kilio kwa wananchi na kwamba ukiwa na bima ya afya kituoni haupati dawa lakini kwenye maduka yao dawa zinapatikana na unalazimika ununue.

ama
ALHAMISI DESEMBA 23, 2021
AFYA NA MAZINGIRA




Ukurasa 12

## Shinyanga vitani kujichomoa kutoka kundi vinara maradhi Ukimwi kitaifa



Ukurasa 13

## UNALIFAHAMU HILI? Kila utajiri mazingira unaojinasibu nao unashikiliwa na hazina misitu

SALAMU ZA UN 2022

# Janga corona liwe darasa haja ya uwekezaji mkubwa kiafya

**Na Mwandishi Wetu**

IKIWA ni muda mfupi kuingia mwaka mpya 2022, huku dunia ikitishwa na janga jipya la maradhi corona, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Dk. Antonio Guterres, anaitaka dunia kutumia janga corona na vita vyake kuwa kigezo muhimu kwa serikali zote kuwekeza zaidi katika mifumo imara ya afya.

Katika ujumbe wake kuhusu Siku ya Kimataifa ya Huduma za Afya kwa Wote inayoadhimishwa Desemba 12 ya kila mwaka, anasema mifumo hiyo ndiyo itaweza kumlinda kila mtu kwa sasa na vizazi vijavyo.

"Janga la corona au Covid 19 limedhihirisha ni jinsi gani ilivyo muhimu kwa nchi zote kuwa na mifumo imara ya afya ambayo inaweza kutoa huduma bora kwa watu wote wakati watakapo zihitaji huduma hizo," anasema.

Pia, anakumbusha namna mwaka jana kulivyoshuhudiwa janga hilo kuvamia mifumo ya afya iliyokuwa imezidiwa uwezo na magonjwa mapya ya mlipuko, ambayo mara nyingi inaumiza maisha ya watu wengi.

Anasema mlipuko corona umedhihirisha kinachoweza kutokea wakati juhudi za kushughulikia majanga kwenye mifumo ya afya, ambayo imeshalemewa kwamba inashindwa kutoa huduma zingine muhimu kama za vipimo na matibabu na chanjo za maradhi mengine, mbali na Covid 19, vivyo hivyo kinamama na watoto.



Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Dk. Antonio Guterres.

"Ni lazima tuongeze juhudi endapo tunataka kufikia lengo la huduma za afya kwa wote ifikapo mwaka 2030" anasema Katibu Mkuu - Dk. Guterres, akikumbusha makubaliano yaliyofikiwa na nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa, Septemba 2019, ilipokuwa miezi michache tu kabla ya kuzuka janga la Covid - 19.

Mkuu huyo wa Umoja wa Mataifa, anasema kufikia lengo hilo kunamaanisha vyema fedha za sekta husika zitumike kuanzia kuwalinda wahudumu afya na kuimarisha miundombinu, hadi kuzuia magonjwa na kutoa huduma za afya karibu na nyumbani kwenye jamii.

"Kuwekeza katika mifumo ya afya, pia kunaimarisha uwezo wa nchi katika kujiandaa na kukabiliana na dharura za afya zitakazojitokeza siku zijazo" anaeleza Katibu Mkuu.

Dk. Guterres anasisitiza kwamba wakati kunapatikana chanjo mpya ya maradhi hayo, vipimo na matibabu ni lazima viwafikie wote ambao wanavihitaji.

"Katika kukabiliana na janga la Covid -19 tumeshuhudia ubunifu wa hali ya juu na haraka katika kufikisha huduma za afya na miundo ya kutoa huduma na pia katika maandalizi. Ni lazima tujifunze kutoka katika uzoefu huu," anaeleza.

"Mwaka 2020 umetukumbusha kwamba afya ni bidhaa muhimu sana duniani. Wakati wa Covid -19 nchi nyingi zimetoa huduma za upimaji na matibabu ya COVID-19 bure kwa watu wao. Wametambua kwamba, uwezo wa kulipia gharama za afya haupaswi kuwa ni tofauti kati ya ugonjwa na afya, kati ya maisha na kifo," anaeleza

Dk. Tedros anasema WHO inazindua mikakati miwili ya kusaidia na kusogeza mbele safari za nchi kuelekea huduma za afya kwa wote.

Kwanza anataja ni mpango wa kimataifa wa kuimarisha huduma za afya ya msingi, kuziwezesha nchi zizuie na kushughulikia dharura za aina zote, kuanzia matatizo binafsi ya shinikizo la moyo hadi milipuko ya virusi vipya vinavyodhuru maisha ya watu wengi.

Pia, anataja lingine ni kuzisaidia nchi ziandae mafungu ya huduma yanazozihitaji kukidhi mahitaji ya kiafya ya watu wao.

Nchini Tanzania tangu mwaka 2007 imekuwa ikitekeleza Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM), ambayo ilianza rasmi mwaka 2008, ikiwamo kufikisha huduma karibu na wananchi, zahanati katika kila kijiji au kitongoji, kituo cha afya kwa kila kata.

Pia inagusa hospitali kwenye kila wilaya na mkoani hospitali za rufani, vivyo hivyo ngazi ya kanda na hadi kitaifa kuna Hospitali ya Taifa Muhimbli, ikiwa na wabia wake kama Taasisi ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu (MOI) na Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, kote na nje ya hapo kukiwapo maboresho ya huduma na kufanyika utafiti wa kina katika maeneo husika.

AFYA

# Shinyanga vitani kujichomoa kutoka kundi vinara maradhi Ukimwi kitaifa

## •Vijana wakabidhiwa rungu la kampeni

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

SHINYANGA imo katika mikoa 15 hapa nchini yenye kiwango kikubwa cha maambukizi ya virusi vya Ukimwi (VVU), ikiwa na kiwango cha asilimia 5.9 ya maambukizi ikilinganishwa na wastani wa Taifa wa asilimia 4.7.

Katika kulikabili hilo, mkoa kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, unaendelea kupambana na kudhibiti maambukizi ya VVU kwa kutoa huduma mbalimbali kwa wananchi kama upimaji afya kwa makundi maalumu ya umma, tiba, matunzo, tohara kwa wanaume na kuhakikisha kondomu zinapatikana.

Kinamama wanatajwa kuongoza kwa ushamiri wa maambukizi hayo, ikilinganishwa na wanaume, pia vijana balehe kutoka Halmashauri za Shinyanga Vijijini, Shinyanga Manispaa, Ushetu, Msalala na Manispaa ya Kahama.

Hapo kunatajwa kuna shida ya wajawazito kuficha taarifa zao za upimaji maambukizi kwa wenzao, hali inayochangia kusababisha ongezeko la ugonjwa huo ndani ya familia, hata vifo visivyotarajiwa.

Imebainika wajawazito wengi wanaopima na kugundulika kuwa na VVU, wanashindwa kuwajulisha wenza kwa kuhofia kupingwa, kunyanyaswa na kuvunjika ndoa, hivyo wanabaki kimya licha ya kuwa kosa kisheria, kueneza ugonjwa ndani ya familia wakati mhusika anajua.




Mabinti kutoka Shirika la SHDEPHA+ wakiwa wameshika kwa pamoja bango lenye ujumbe kutoshiriki ngono zembe. **PICHA ZOTE: SHABAN NJIA.**

### MGANGA WA MKOA

Dk. Yudas Ndungile, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, anasema mkoa umejipanga kuhakikisha asilimia 95 ya wanaoishi na VVU wanatambua hali zao za maambukizi na hadi Septemba mwaka huu walikuwa asilimia 84.6

Anasema wamekuwa wakiongeza vituo vya kutoa huduma za matunzo na tiba (CTC) kwa wanaoishi na Ukimwi, kutoka asilimia 63 hadi kufikia 85 katika halmashauri zote kufikia Septemba mwaka huu na walikuwa na wateja 67,911 kulinganisha na mwaka jana kipindi kama hiki ambapo walikuwa 66,789.

Daktari huyo anafafanua, hadi kufikia Septemba mwaka huu zaidi ya wateja 18,256 walipotea kwenye huduma na kati yao 1,238 walitafutwa na kurejeshwa kwenye huduma, sasa wanaendelea vyema na matumizi ya dawa za kufubaza maambukizi hayo.

Pia, anasema wanaendelea kutoa huduma zinazohusu Ukimwi mahali pa kazi kwa taasisi za serikali na zisizo za kiserikali kutoa elimu ya maambukizi, pia namna ya kujikinga, upimaji na elimu sahihi ya matumizi ya kondomu na kuzigawa na zaidi ya kondomu 17,500 zimesambazwa kwenye taasisi za umma 25,300.

### VVU MKOANI

Dk. Ndungile anasema, mwaka jana walipima VVU watu 259,450 na kati yao 10,286 waligundulika kuwa na maambukizi, wanaume walikuwa 4170 na wanawake 6118 sawa na asilimia 3.9 anasema ushamiri huo wa VVU unatokana na wajawazito kutotoa taarifa kwa wenzao, baada ya kupima na kubainika wana maambukizi.

Anasema mwaka huu kuanzia Januari hadi Novemba, waliwapima wateja 148,345 kati yao wanaume walikuwa 63,914 na wanawake 84,431, wateja 6705 waligundulika kuwa na maambukizi hayo, wanaume wakiwa 2739 na wanawake 3966 sawa na asilimia 4.5 ikilingashwa na mwaka jana.

"Tumeongeza idadi ya vituo vya upimaji wa VVU na ushauri kutoka 137 hadi 246 mkoa mzima, lakini changamoto tuliyo nayo ni wajawazito wanaogundulika kuwa na maambukizi kutowaambia wenza wao, ili wote kwa pamoja wapate ushauri wa namna ya kumtunza mtoto angali bado tumboni asipate maambukizi," anasema Dk. Ndungile.

### CHANGAMOTO/WITO

Dk. Ndungile anasema, bado wanakutana na changamoto katika utoaji huduma, ikiwamo wateja kushindwa kujitokeza kwa wingi kupata dawa na wengine kuhama vituo bila taarifa, akitaja idadi ya vituo vya huduma za tiba na matunzo havitoshi kukidhi idadi ya wananchi wake, kwani vituo 85 (34.5%) tu vinatoa huduma, kati ya 246 vinavyohitajika.

Pia, anasema ushiriki mdogo wa wanaume kwenye huduma za kuzuia maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto, inajumuisha wajawazito kuwa wasiri baada ya kubainika kuwa na VVU , wakishindwa kuwashirikisha wenza wao kutokana na hofu ya kufanyiwa ukatili na kuvunjika kwa ndoa.

Dk. Ndungile anawataka wananchi kuacha mila potofu ya dawa za kufubaza VVU ili kupunguza wateja wanaopotea kwenye vituo vya kutoa huduma na kuwa wawazi, kuhusu hali za afya yao hasa wanafamilia, ili kuongeza ufuasi wa dawa za ARV.

### SHDEPHA+/KATIBU TAWALA

Mratibu wa Afya na Upimaji Mradi wa Ukimwi na Kifua Kikuu wa shirika la SHDEPHA+ Dk. Bakari Omary anasema kutokomeza janga hilo wamejikita katika utoaji elimu ya afya ya uzazi wa mpango kwa mabinti balehe chini ya mradi wa Epic, ili kutambua athari za ugonjwa huo.

Pia, anasema wanayafikia makundi maalumu elimu ya ukatili wa kijinsia upimaji na uwezeshaji kiuchumi kwa kuwapatia ujuzi ikiwamo ufundi cherehani, saluni na magari ili wasijiingize kwenye biashara ya kuuza miili yao na kupata maambukizi.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Shinyanga, Zuwena Omary, anasema lengo la kuadhimisha Siku ya Ukimwi Duniani, ni kukumbushana uwapo wa ugonjwa huo, kupima, matumizi sahihi ya dawa za ARV na kuendelea kuchukua tahadhari.

Anawataka wananchi kupinga ndoa za ututoni, kurithisha wake na kujihusisha kwenye mapenzi ingali wakiwa na umri mdogo ili kujikinga na ugonjwa huo na kuwasihi wajawazito kuwapatia taarifa waume zao kama wamegundulika na VVU na kumlinda mtoto aliyeko tumboni na maambukizi.

### MAAMBUKIZI KWA UMMA

Mkazi wa kata ya Isaka, Halmashauri ya Msalala, Sada Ramadhani, anasema elimu ya matumizi sahihi ya dawa za kufubaza maambukizi inahitajika vijijini, kwa sababu wananchi wengi wanapata maambukizi na wanakimbilia kwa waganga wa jadi kutafuta tiba, wakiamini wamerogwa badala ya kwenda katika vituo vya afya.

Godfrey Michael, anashauri wataalamu kuwapatia elimu ya kutambua dalili za ugonjwa wa Ukimwi waganga wa jadi, ili watakapopata wateja wa namna hiyo, wawashauri kwenda kwenye vituo vya afya kwa matibabu zaidi.

Aidha, Felister John, mkazi wa kata ya Majengo, anasema yeye ni miongoni mwa wananchi waliougua ugonjwa wa kifua kikuu na kukimbilia kwa mganga wa jadi, lakini mganga alimshauri na kumtaka kwenda hospitali kupata tiba ambapo mpaka sasa anaendelea na matibu vema.



Katibu Tawala wa Mkoa wa Shinyanga, Zuwena Omary, akizungumza na wananchi wa kata ya Isaka, Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga (hawapo pichani) katika Maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani hivi karibuni, yaliyoambatana na uchangiaji wa damu, tohara, upimaji wa VVU na chanjo ya Uviko-19.

MAZINGIRA

## UNALIFAHAMU HILI?

# Kila utajiri mazingira unaojinasibu nao unashikiliwa na hazina misitu

## •Ardhi, maji, hewa, chakula...matambiko

**Na Dk. Felician Kilahama,**



Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Deo Ndejembi alipozungumza na wananchi wa kata ya Njoge. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

MSITU ni mhimili wa kiuchumi, kimazingira na kijamii, ambao ni muhimu kwa maisha ya umma. Pia, iko mtambuka kwa sekta nyingine kama inavyofafanuliwa katika makala hii.

Katika makala ya Alhamisi iliyopita nilieleza eneo la msitu wa asili ni hekta 33.5 milioni na nusu yake imehifadhiwa kisheria, kwa takwimu za Mradi wa Kupima na Kutathmini Misitu Nchini (NAFORMA) za 2015, eneo lilili na misitu ni hekta 48.1 milioni, ikiwa ni ongezeko la takribani hekta milioni 14.6.

Tafsiri ya neno 'msitu' iliyowasilishwa Umoja wa Mataifa inafafafnu: "Ni eneo lenye miti yenye urefu wa kuanzia mita mbili na matawi yake (crown cover) kufunika asilimia 10 ya hekta moja."

Kabla ya hapo, msitu ulijulikana kuwa eneo lenye miti mirefu zaidi ya mita tano. Kwa tafsiri ya sasa maeneo mengi yaliyofunikwa na vichaka yakatambulika kuwa ni maeneo yenye misitu.

Wengi huiangalia misitu na miti ya kupandwa kwa kuzingatia zaidi upatikanaji magogo, mbao, kuni, mkaa, nguzo na malighafi kwa viwanda na kwa kiasi kikubwa ukweli unabaki kushika maisha ya Watanzania mijini na vijijini.

### KILIMO CHA KIJANI

Inaopongelewa kilimo kijani, misitu inachangia kurutubisha ardhi na udongo kutokana na majani, matawi na miti inayozeeka kuanguka na hatimaye inaoza hata kutengeneza mbolea asilia.

Msitu unahifadhi nyuki, ambao wanasaidia kutengeneza asali na katika kulitimiza hilo, nyuki hutembelea maua ya miti au mimea mingi kutafuta 'nekta' hivyo kueneza 'poleni' kwenye maua.

Kwa kufanya hivyo, husaidia mavuno ya chakula na biashara kuongezeka kupitia urutubishaji maua (cross pollination) ikiwa ni huduma muhimu ya kiikolojia kwa wakulima.

Uzoefu unaonyesha penye misitu ya asili, kunakuwapo juu na chini ya ardhi, wadudu na viumbe mbalimbali vinavyosaidia kufanya majani, au twangamotaka nyingine, kuweza kuoza haraka na kuchanganyika na udongo hivyo kuwepo rutuba ya kutosha.

Vilevile, misitu husaidia kuhifadhi ardhi kwa kupunguza kasi ya maji ya mvua au upepo mkali hivyo kuzuia mmomonyoko wa udongo. Wakulima wengi wanafahamu thamani ya udongo wenye mboji, ndiyo maana hukimbilia kufyeka maeneo yenye misitu kwa ajili ya kilimo cha kuhamahama ili waweze kupata mazao mengi bila kuingia gharama za kutumia mbolea ya viwandani.

Isitoshe maeneo ya misitu husaidia udongo uwe na unyevunyevu kwa muda mrefu zaidi ukilinganisha na maeneo yaliyo wazi. Kadhalika, zipo aina mbalimbali za miti ambazo mizizi yake hurutubisha udongo kwa kutumia naitrojeni toka hewani na kuiingiza ardhini. Miti hiyo ni kama viwanda na hutengeneza mbolea ardhini hivyo kuboresha mazao ndiyo maana tunashauri kilimo - misitu kizingatiwe.

Rasilimali misitu, pia ni nyenzo muhimu kwa chakula na maji kwenye misitu, hasa nyakati za ukame mifugo huchungiwa kwenye misitu.

Misitu ya asili pia inachangia usalama wa chakula, kwa kuzingatia upatikanaji matunda asilia, kama ukwaju, ubuyu na mboga asilia.

Ni maeneo yanayohifadhi na kutunza wadudu mbalimbali wanaoliwa, uyoga na makazi ya viumbehai mbalimbali, ikiwamo wanyamapori ambao ni mlo kwa wengine. Mazao ya misitu huuzwa na pato linatumika kununua chakula, vilevile misitu ni chanzo muhimu cha kupata dawa za asili zinazotibu magonjwa mbalimbali.

Duniani, viwanda vingi msingi wake muhimu ni misitu kwa wastani wa asilimia 75, ndio inatoa vinasaba vya dawa na vipodozi ambavyo hutokana na misitu au miti na mimea. Kwa hali ilivyo, sekta ya afya na tiba inafungamana sana na uwapo wa misitu.

### MAJI & HEWA

Kwa upatikanaji maji, misitu inachangia kwa kiasi kikubwa. Maeneo yasiyo na misitu hubaki na ukame sana, maji yanapatikana kwa shida.

Kiikolojia, misitu kwenye maeneo yenye miinuko husababisha upepo wenye unyevu kutoka baharini, kupungua kasi yake na hatimaye inatengeneza mawingu na yanapokuwa mazito, mvua inanyesha.

Mara zote, mvua inaponyesha, maji huweza kuingia kirahisi ardhini na hatimaye kuwa chanzo kikuu cha mito. Mfano, misitu katika milima ya Uluguru ni chanzo muhimu cha Mto Ruvu. Pia, mito mikubwa nchini vyanzo vyake vikuu ni katika misitu iliyo katika Milima ya Tao la Mashariki.

Misitu ni uhai, kwa maana inazalisha hewa safi ya oksijeni ambayo watu wanaivuta kila siku siku. Binadamu anapopumua hutoa gesiukaa ($CO_2$) na miti huitumia na kisha inatoa oksijeni ($O_2$), ambayo ni msingi wa uhai wa binadamu na mnyama.

### MAHITAJI MENGINE

Kukosekana matumizi endelevu ya misitu, kunazua hatari nyingine kwenye uhai wa wanyama, pamoja na ustawi wa utalii, kwa sababu iko wazi wanyamapori wanapoathirika kwa kukosa chakula na maji, iko wazi utalii kitaifa utayumba na kuangukia pengo la kiuchumi.

Vilevile, katika taasisi za kitaaluma, nako misitu inatumika kufundisha wataalamu (hasa wa kisayansi) kwa njia ya vitendo, mambo mbalimbali kama mbinu za uhifadhi na utafiti kwa manufaa ya umma.

Isitoshe, misitu inatajwa kuwa sehemu muhimu sana katika mazingira yanayomzunguka binadamu na wanyama. Dunia sasa inalia na changamoto ya ongezeko la joto na mabadiliko ya tabianchi kutokana na shughuli mbalimbali za binadamu zisizo endelevu viwandani na misituni.

Nchi zilizoendelea zinatajwa kuwa wachangiaji wakubwa wa gesiukaa angani na mimea mingine, hivyo kuwapo kiwango kikubwa angani kinachotishia uhai wa umma.

Athari za mabadiliko ya tabianchi ni nyingi ikiwamo kuongezeka ukame, kuzuka wadudu na magonjwa yanayodhuru mimea, mazao, wanyama na binadamu kuongezeka, hata kutishia uhai.

Mara zote huwa kunafanyika juhudi kubwa za kuhifadhi misitu na kupanda miti, kwa faida endelevu ya vizazi. Huwa ni chanzo muhimu cha nishati kwa taifa, kwa sababu inachangia upatikanaji maji ya kuzalisha umeme, ikiwa ni pamoja na asilimia 80 ya nishati inayotumika nchini kupitia kuni na mkaa.

Pia, ni rasilimali muhimu vijijini ambako makabila mbalimbali hutumia misitu ya asili kwa matambiko na masuala ya kimila/kifamilia ikiwamo sehemu za kuabudu, hadi maeneo ya kuzika.

### MISITU INAVYOTOWEKA

Hata hivyo, inabaki ukweli kuwa kuwapo kasi ya kutoweka misitu na uoto wa asili kwa kasi kubwa (wastani wa hekta 372,000 hadi 500,000 kwa mwaka), inatokana na misitu kutopewa umuhimu wa kutosha kama ilivyo mfano katika sekta za afya, maji, elimu, kilimo, miundombinu.

Namna sekta hizo zinagusa maisha ya Watanzania, misitu nayo inagusa maisha ya Watanzania. Kimsingi, misitu ya asili haijasimamiwa ipasavyo, kutokana na uhalisia unaotawala.

Hali ya misitu nchini siyo nzuri na madhara yake kwa umma yako juu, ikitoa mwanya kwa wataalamu, wazidi kubeba jukumu la haja ya kuchukuliwa hatua za kuiunganisha misitu na sekta muhimu za kitaifa, kuhakikisha rasilimali hiyo inabaki kuwa na umuhimu wa kudumu kwa wananchi waoimiliki.

***Mwandishi ni Mkurugenzi wa Misitu na Nyuki Mstaafu***



Eneo la hifadhi katika kata ya Njoge, ambako kumepigwa marufuku kutumika kwa malisho ya mifugo na kilimo.

AFYA

# Mkurugenzi UNICEF: Tufanye tunavyoweza shule zisifungwe kwa shinikizo la Covid 19

- Yajue yanayowakuta watoto makwao
- UN yawatungia kitabu cha ushuhuda



Wataalamu wa afya wa Umoja wa Mataifa, wakiendelea na kampeni nchini DRC, kuhimiza chanjo dhidi ya corona.

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI wagonjwa wa corona wakiongezeka duniani, kukichochewa na aina mpya ya kirusi omicron, serikali nyingi duniani zinatajwa kufikiria uamuzi wa kufunga shule, kama njia mojawapo ya kupunguza kusambaa maambukizi.

Lakini, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) Henrietta Fore anapingana mno na hoja hiyo, akiwa na maoni kwamba nchi zinapaswa kuhakikisha ufungaji shule ni suala la mwisho na kufungua liwe jambo la kipaumbele.

Anaeleza kuna mambo mengi yanayoendana na uamuzi wa kufunga shule, ikiachiliwa mbali wanafunzi kupoteza muda wa kusoma, kuna mengine kama ugumu wa namna ya kufikiwa huduma za afya na mlo wao.

"Kizazi hiki cha watoto wa shule kwa pamoja kinaweza kupoteza jumla ya (fedha) dola trilioni 17, ndio maana kufungwa kwa shule kote nchini kunapaswa kuepukwa kila inapowezekana.

"Wakati maambukizi ya covid 19 yanapoongezeka na hatua madhubuti za afya ya umma kuwa jambo la lazima, shule lazima ziwe sehemu za mwisho za kufungwa na za kwanza kufunguliwa tena," anasisitiza Fore.

Anafafanua kuwa wanafahamu lazima zichukuliwe hatua za kupunguza maambukizi shuleni, ila katika utekezaji wake kunapaswa yatumike maarifa stahiki kuhakikisha masomo yanaendelea.

Mkuu huyo wa UNICEF, anafafanua "Pia, tuongeze uwekezaji katika kuwaunganisha kidigitali, ili kuhakikisha kuwa hakuna mtoto anayeachwa nyuma mwaka 2022, hauwezi kuwa mwaka mwingine wa masomo yaliyotatizika. Mwaka huo mpya unahitaji kuwa mwaka ambao elimu na maslahi bora ya watoto, yanatangulizwa."

**UNDANI WA RIPOTI**

Ripoti mpya iliyotolewa UNICEF inasema janga la Covid 19 limeleta hali mbaya zaidi kwa watoto kuwahi kushuhudiwa katika historia yake ya miaka 75 na inazitaka nchi kuongeza juhudi za kuwanusuru.

Inahimiza kuwapo hatua ya haraka kubadili athari mbaya ya maradhi hayo kwa watoto na vijana, ikisema katika miaka miwili ya janga la corona limedidimiza zaidi na kuwaweka watoto hatarini, kwa kuwaongezea changamoto za umaskini, lishe, afya ya akili na kukosekana usawa.

Akisoma ripoti hiyo jijini New York, Marekani Mkurugenzi Mtendaji wa UNICEF, Henrietta Fore anasema licha ya historia yao nzuri ya kuunda mazingira bora na salama kwa watoto duniani yenye matokeo chanya kwa mamilioni, sasa hali inabadilika.

"Wakati idadi ya watoto walio na njaa, walio nje ya shule, walionyanyaswa, wanaoishi katika umaskini au kulazimishwa kuolewa ikiongezeka," analalamika.

"Idadi ya watoto wanaopata huduma za afya, chanjo, chakula cha kutosha na huduma muhimu inapungua. Katika mwaka ambao tunapaswa kutazamia mbele, tunarudi nyuma," anasema.

Takwimu zilizotolewa katika ripoti hiyo, imo inayoonyesha watoto zaidi ya milioni 100 wanaokadiriwa kuishi katika umaskini mbalimbali, ikiwa ni ongezeko la asilimia 10 tangu mwaka 2019.

"Katika enzi hizi za janga la corona kuendelea kuongezeka kwa migogoro, hali ya mabadiliko ya tabianchi kuzidi kuwa mbaya kunahitajika uangalizi wa karibu zaidi wa watoto.

"Tupo njia panda. Tunapofanya kazi na serikali, wafadhili na mashirika mengine ili kuanza kupanga njia yetu ya pamoja kwa miaka 75 ijayo ni lazima tuwaweke watoto mbele kwenye mipango ya uwekezaji" Mkurugenzi huyo anasisitiza.

Ripoti hiyo inapendekeza mambo ya kufanyika, ikiwamo uwekezaji zaidi katika kuwalinda watoto na kuwapatia lishe bora.

**MADHILA KWA WATOTO**

Katika mandhari ya nchi mbalimbali na hasa zinazokabiliwa na majanga kama hali ngumu ya uchumi, pia mapigano au machafuko ya namna mbalimbali, mfano hai nchini Msumbiji.

UNICEF inasema hali ni mbaya kwa afya ya watoto katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), hata wanakijiji wanalazimika kupigania mazao ya kusaidia kuzuia utapiamlo.

Kutokana na vikundi vilivyopewa kipaumbele kwa ajili ya chanjo dhidi ya Covid 19, serikali ya Uganda imeanza kutumia mbinu ya kuwachanja walio tayari ikijumuisha kwenye maeneo ya ibada, hafla na mitaani waliko, wanakuwa tayari iwapo wanaalikwa .

**WATUNGIWA KITABU**

Shirika la UNICEF limeandaa kitabu kipya cha watoto kilichopewa jina 'Shujaa Wangu ni Wewe 2021' ambacho kimezinduliwa mwishoni mwa wiki na mashirika ya kibinadamu ikiwamo Umoja wa Mataifa, kinawalenga zaidi wenye umri kuanzia miaka 16.

Inatajwa katika taarifa ya pamoja ya Umoja wa Mataifa na UNICEF, lengo la kitabu ni kuwapa watoto matumaini ya kuendelea na maisha, hasa wakati wa janga la corona.

Inatajwa kitabu hicho ni kazi ya ushirikiano wa vyombo 60 kutoka sekta za kibinadamu, Shirika la Afya Duniani (WHO) na UNICEF, kikiwalenga wazazi, walimu na wataalamu wa afya katika madhumuni ya kuwafundisha watoto jinsi ya kukabiliana na maradhi Corona.

Ni dhana inayogusa maeneo kama vile elimu na burudani na muda wanaoutumia na marafiki, ikitiliwa maanani hadi sasa wengi katika umma wanaathirika na janga hilo katika mustakabali huo, pia familia husika na walimu shuleni.

Kitabu hicho ni matokeo ya ushirikiano wa mashirika 60 katika sekta ya kibinadamu, yakijumuisha mashirika ya Umoja wa Mataifa ya WHO, UNICEF na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR).

Mhusika mkuu ni Arius, kiumbe wa kupendeza ambaye anasafiri kote duniani akisaidia watoto kupata tumaini la siku za usoni na furaha katika mambo rahisi.

Mkurugenzi Mkuu wa WHO, Tedros Ghebreyesus, anasema kitabu hicho kitasaidia kufundisha watoto kujenga mwelekeo na hali ya matumaini kwa siku za usoni.

***Makala hii ni kwa mujibu wa vyanzo mbalimbali, vikiwamo taarifa rasmi za UNICEF wiki hii.***



Uhalisia wa hamasa ya uvaaji barakoa katika makundi yote, watoto na wakubwa nchini DRC. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**





# Machinga kicheko kwa kupatiwa eneo

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MACHINGA jijini Dodoma wameipongeza serikali na uongozi wa jiji kwa kuwajengea mradi mkubwa wa soko la wazi litakalowawezesha kufanya biashara zao kwa saa 24.

Soko hilo ambalo linalojengwa eneo la Bahi Road pia litawawezesha kuondokana na kero ya kufanya biashara kwenye maeneo yasiyo rasmi na hatarishi pamoja na kuliweka jiji kwenye mazingira safi kwa muda wote.

Mwenyekiti wa Umoja wa Machinga Dodoma, Bruno Mponzi, alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya jiji kuingia mkataba wa mradi huo wa ujenzi na kampuni ya Mohamed Builders utakaogharimu Sh. bilioni 7.5 hadi kukamilika kwake.

Pamoja na pongezi hizo, kupitia soko hilo, machinga watakuza mitaji yao na baadaye kuingia kwenye ngazi ya wafanyabiashara wakubwa na hatimaye kupata mikopo toka taasisi za kifedha.

Pia serikali itakusanya mapato yao kwa urahisi tofauti na ilivyo sasa ambapo machinga wamezagaa kwenye maeneo mbalimbali bila utaratibu.

"Sisi machinga wa Dodoma tuna kila sababu ya kuipongeza serikali kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji kwa hatua yake ya kutujengea mradi huo wa soko la wazi ambao unaoonekana kutengua kitendawili cha muda mrefu," alisema.

Mstahiki Meya wa Jiji la Dodoma, Prof. Davis Mwamfupe, akizungumza na machinga hao kwenye utiaji wa saini huo, aliwataka kutumia uwapo wa soko hilo kukuza mitaji kwa malengo ya kujiinua kimapato na kuingia kwenye soko la ushindani kutokana na bidhaa zao.

# Kikao cha waziri chachambua afya ya mama na mtoto

**ibua Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsi, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, ameongoza kikao cha wataalamu wa afya nchini wakiwamo madaktari bingwa, waganga wakuu wa mikoa, wilaya na hospitali zote kikihusisha kamati ya kitaifa ya kufuatilia vifo vya wazazi vinavyotokea kila siku.

Aidha, kikao hicho kilikuwa na lengo la kujadili na kuchambua taarifa za vifo vilivyotokea kutokana na sababu za uzazi.

Kikao hicho kilichofanyika kwa njia ya mtandao, Dk. Gwajima aliongoza kikiwa sehemu ya mkakati wa wizara kuhakikisha kila kifo cha mzazi na mtoto mchanga kinafanyiwa tathmini ya kitaifa ndani ya saa 24.

Kutokana na kikao hicho moja ya vituo vilivyoripoti vifo kwa juzi ni pamoja na zahanati ya Songambele katika Halmashauri ya Buhigwe mkoani Kigoma. Dk. Gwajima alimpongeza muuguzi Nyanduni Joachim na timu yake kwa kupigania maisha ya mzazi ambaye alichelewa kufika kituoni kwa kuokoa maisha ya mtoto na mama.

Dk. Gwajima alitoa wito kwa wananchi kuhakikisha wanasikiliza ushauri wa wataalamu wa afya ili wawahi kufika kwenye vituo vya kutoa huduma kwa wakati hali itakayotoa fursa kwa wataalamu kutumia taaluma zao kuokoa maisha.

Alisema wizara imeimarisha ufuatiliaji wake kwa msaada wa teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) ili kufikia kila kituo cha kutoa huduma za afya, hivyo wananchi wasiwe na wasiwasi na huduma zinazotolewa.

Pia wananchi walitakiwa kutoa ushirikiano na taarifa kwa wakati ili kama kuna uzembe wowote ambao haujabainika uibuliwe na kuzuiwa.

Alisema vifo vya wazazi na watoto wachanga havikubaliki na kwa kila kifo uchambuzi utafanyika mubashara ili kujiridhisha kuwa kilikuwa kinaepukika au hapana na kama juhudi stahiki zilifanyika kwa wakati na mapitio ya vifo yataonyesha kuimarishwa ili kufikia vifo vyote nje vya uzazi na watoto wachanga.

Dk. Gwajima alitoa wito kwa wananchi kutoa ushirikiano wao wa taarifa za kuridhika au kutoridhika kwa huduma kupitia namba za viongozi wa ngazi ya kituo, halmashauri na mkoa zilizobandikwa kwenye mbao za matangazo yao, pia wanaweza kuwasilisha moja kwa moja wizarani.

Dk. Ahmad Makuwani, daktari bingwa wa magonjwa ya kinamama akiungana na mabingwa wengine kutoka hospitali mbalimbali za rufani za mikoa na kanda pamoja na hospitali za halmashauri, vituo vya afya na zahanati, alimhakikishia waziri kuwa ataratibu usimamizi endelevu wa mkakati huo ambao umeonyesha kuwa na tija.




Katibu Tawala Mkoa wa Dodoma, Dk. Fatuma Mganga, akizungumza na baadhi ya viongozi wa vikundi vya uzalishaji uchumi Mkoa wa Dodoma alipokutana nao ofisini kwake jijini humo jana kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kuongoza wengine. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Aagiza kampuni kuendelea kuchenjua madini

**N Renatha Msungu,** BAHI

WAZIRI wa Madini, Dk. Doto Biteko, ameitaka Kampuni ya Uchenjuaji Madini ya Dhahabu ya Binsulum Mine, kuanza uchenjuaji baada ya kukosa kibali cha mazingira kutoka Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa kipindi cha miaka miwili tangu ilipoomba.

Dk. Biteko alitoa agizo hilo wilayani Bahi, Dodoma baada ya kutembelea mgodi wa Binsulum ulioko katika kijiji cha Nholi Kata ya Mpalanga. Alisema ofisi yake itashirikiana na NEMC ili kibali cha mazingira kipatikane haraka wakati kampuni hiyo ikiendelea na shughuli za uchenjuaji.

Pia alisema serikali ina mpango wa kufanya utafiti na kuongeza vituo vya mfano vya uchenjuaji madini katika maeneo mbalimbali ikiwamo Wilaya ya Bahi baada ya kuona uhitaji mkubwa wa mafunzo kwa wachimbaji wadogo.

Biteko alimtaka Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Mkunda, kushirikiana na Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Dodoma kutafuta eneo ili kifunguliwe kituo cha kuuzia madini katika eneo la Nholi ili kuwapunguzia adha wachimbaji wadogo kwenda kuuza mbali.

Sambamba na hilo, aliwapongeza wachimbaji wadogo wa Nholi kwa juhudi za uzalishaji mkubwa wa dhahabu. Alisema zaidi ya asilimia 90 ya madini yote yanayouzwa katika soko la madini la mkoa wa Dodoma yanatoka katika eneo hilo.

Waziri pia alitumia fursa hiyo kuwaonya wote ambao bado wanatorosha madini na kuwataka wachimbaji wote kuwa walinzi wa rasilimali hiyo.

"Wako baadhi ya watu bado wanatorosha madini. Mtu yoyote anayetorosha madini tumchukie tena ikibidi tuwaeleze vyombo vya ulinzi na usalama kwamba kuna mjanja mjanja anatorosha madini hapa ili wamfanyie kazi," alisema.

Dk. Biteko pia iliwataka wachimbaji wadogo wa madini wa Nholi kuhakikisha wanachimba kwa usalama na kuzingatia usalama mahali pa kazi ili kulinda afya za watu.

Mbunge wa Bahi, Kenneth Nollo, alieleza changamoto zilizoko katika eneo hilo na kumwomba Waziri Biteko kuchangia ujenzi wa shule na kituo cha polisi ili watoto waende shuleni na kusaidia ulinzi katika eneo hilo.

Meneja wa mradi wa uchenjuaji dhahabu, Mohamed Nassor, alisema zaidi ya wafanyakazi 50 wamesimamishwa kazi kutokana na kukosekana kwa kibali kutoka NEMC licha ya kuomba miaka miwili iliyopita.





# Wanafunzi vyuo vikuu wachangia ujenzi wa shule ya sekondari kata

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANAFUNZI wa vyuo vitatu vya elimu ya juu wameamua kuunga mkono nguvu za wananchi wa kata hiyo kwenye ujenzi wa shule mpya ya sekondari katika Kata ya Itende jijini Mbeya.

Wanafunzi hao ni kutoka Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) Kampasi ya Mbeya na Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Uyole. Wanafunzi hao mbali na kuchangia vifaa pia walichangia nguvu kazi.

Ofisa Elimu wa Kata ya Itende, Mwalimu Japhet Katitu, alisema hayo jana alipokuwa anapokea mchango wa vifaa mbalimbali vya ujenzi kuwa wanafunzi hao wameamua kufanya hivyo kutokana na kata hiyo kukosa shule ya sekondari.

Kukosekana kwa shule hiyo, alisema kulisababisha wanafunzi wanaofaulu mitihani ya darasa la saba na kuchaguliwa kujiunga na masomo ya sekondari, kutembea umbali wa zaidi ya kilomita mbili kwenda kusoma katika Kata ya Iwambi.

Mwalimu Katitu alisema watoto wanaofaulu elimu ya msingi katika kata hiyo, wanalazimika kwenda kusoma Iwambi hali ambayo inasababisha vikwazo vingi kwa wanafunzi vikiwamo utoro na vishawishi.

Alisema kutokana na tatizo hilo, wananchi wa kata hiyo waliamua kujenga shule mpya kwa kuchangishana michango na kwamba mpaka sasa wamekamilisha ujenzi wa vyumba sita vya madarasa na ofisi moja.

Majengo hayo, alisema yamefikia hatua ya umaliziaji na kwamba wanatarajia mpaka kufika Januari shule zitakapokuwa zinafunguliwa, vyumba vyote viwe vimekamilika.

Alisema Halmashauri ya Jiji la Mbeya imechangia Sh. milioni tatu kwa ajili ya kukamilisha baadhi ya vyumba hivyo huku baadhi ya wadau pia wakichangia michango mbalimbali.

"Tunashukuru pia kwa siku ya leo (jana) wahitimu hawa wa vyuo wamekuja kutuunga mkono. Wametuletea vifaa vya ujenzi, lakini pia wamekuja na mafundi wao ambao watatusaidia kuongeza nguvu hapa. Wakati wa masika, watoto wengi walikuwa wanashindwa kwenda shuleni kwa sababu hakuna vivuko vya uhakika," alisema Katitu.

Mwenyekiti wa msafara wa wanafunzi hao, Rashid Msalilwa, alisema waliamua kuungana kuchangia ujenzi wa vyumba vya madarasa ili kuunga mkono juhudi za wananchi kwenye ujenzi wa shule hiyo.

Alisema wanataka kushirikiana na wananchi wa Kata ya Itende ili kuhakikisha wanafunzi wote wanaotakiwa kujiunga na masomo ya sekondari Januari, waanze bila kuwapo vikwazo vya aina yoyote.

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, waliamua kwenda na mafundi ujenzi kutoka MUST ambao wamebobea kwenye ujenzi ili kusaidia mradi huo kukamilika haraka.

"Tutaendelea kuwashawishi na wanafunzi wa vyuo vingine vya mkoa huu pamoja na wadau wengine wachangie mradi hu una mwezi Januari wadogo zetu zetu waanze masomo," alisema Msalilwa.

Naye Gaina Mhando aliwaomba wanafunzi wa vyuo vingine waendelee kuchangia miradi mbalimbali ikiwamo hata ya afya kwenye maeneo yao akidai kuwa ni sehemu ya kurudisha fadhila kwenye jamii.



Baadhi ya vijana wa Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), wakiendelea kuchapia baadhi ya majengo ya Shule ya Sekondari ya Kata ya Itende jijini Mbeya kwa lengo la kuwaunga mkono wananchi wa kata hiyo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Walalamika kukosa maji kwa siku tatu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI wa Bonde la Uyole jijini Mbeya wamelalamika kukosa huduma ya maji kwa siku ya tatu mfululizo huku Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-WSSA) ikishindwa kutoa taarifa kuhusu tatizo hilo.

Wakizungumza na Nipashe jana, baadhi ya wananchi hao walisema wanalazimika kwenda kutafuta huduma hiyo maeneo ya kwenye mito na kununua kwa baadhi ya vijana wanaotembeza kwenye matoroli na kwamba gharama imeongezeka.

Mmoja wa wananchi hao, Halima Mwasote, alisema kwa sasa wananunua dumu la maji kwa Sh. 500 jambo ambalo walikuwa wameshalisahau kwa muda mrefu na kwamba tatizo hilo limeongeza gharama za maisha kuwa juu.

"Kama unavyoona haya mabomba hapa ni siku ya tatu maji hayatoki kabisa, tulikuwa tumezoea maji kukatika na kurejea lakini sasa hivi imekuwa tatizo kubwa mno, tunaomba watusaidie maana imekuwa kero sasa," alisema Halima.

Naye Mpoki Mwanyanje, ambaye anamiliki mgahawa, alisema kukatika kwa maji kumewaongezea gharama za uendeshaji wa biashara kutokana na kutumia gharama kubwa kununua maji hayo kutoka kwa vijana.

Aliiomba Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya kulishughulikia tatizo hilo haraka ili kuwaondolea kero hiyo na kwamba kuna hatari magonjwa ya mlipuko kwa maelezo kuwa hawana uhakika na usalama wa maji wanayonunua.

Ofisa Uhusiano wa Mbeya -WSSA, Neema Stanton, alikiri kukosekana kwa huduma hiyo katika bonde lote la Uyole na kwamba chanzo ni kutokana na hitilafu ya umeme kwenye mitambo ya kusukuma maji katika chanzo cha Nsalaga.

Alisema wataalamu wa mamlaka hiyo wanaendeela kushughulikia tatizo hilo ili kurejesha huduma kwa wananchi na hivyo akawataka wananchi kuwa na subira wakati tatizo hilo likishughulikiwa.

# Mbunge amwangukia waziri ujenzi wa bweni

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MBUNGE wa Mbeya Vijijini, Oran Njeza, ameiomba serikali kujenga bweni kwa ajili ya wanafunzi wa kike katika Shule ya Sekondari Usongwe iliyoko katika Mji wa Mbalizi ili kuliepusha kundi hilo na mazingira magumu.

Alitoa ombi hilo juzi wakati wa ziara ya Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, ambaye alikuwa anakagua maendeleo ya ujenzi wa miundombinu ya shule kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha kwanza mwakani.

Njeza alisema Shule ya Sekondari ya Usongwe iko katikati ya mji wa Mbalizi na ina zaidi ya wanafunzi 2,500 kuanzia kidato cha kwanza mpaka kidato cha sita lakini haina miundombinu ya kutosheleza mahitaji ya wanafunzi wanaokaa bweni.

Alisema wanafunzi wanaokaa bweni ni wa kidato cha tano na sita ambao wote ni wa kike, lakini kutokana na kukosekana kwa mabweni baadhi ya vyumba vya madarasa vimegeuzwa kuwa mabweni hali ambayo alisema si sahihi.

Miundombinu yote ya shule hiyo, alisema imejengwa kwa nguvu za wananchi wa Mbalizi na mpaka sasa wanaendelea na ujenzi wa miundombinu mingine ikiwamo ya ukumbi wa mikutano ambao pia utatumiwa na wanafunzi kufanyia mitihani na kulia chakula.

"Hii shule kuna watoto wetu wa kike wanaishi hapa, sasa ukiangalia hata wigo uliopo hapa sio imara kwa usalama wa mabinti zetu, hivyo tunakuomba Naibu Waziri utusaidie angalau serikali ituunge mkono kwenye miradi hii," alisema Njeza.

Alisema serikali ilitoa fedha hivi karibuni ambazo zilikuwa kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya elimu lakini bado wana uhitaji mkubwa kutokana na miundombinu mingi kuendelea kuhitajika.

Akijibu maombi ya mbunge, Silinde alisema serikali itahakikisha inawaunga mkono wananchi hao ili kukamilisha baadhi ya miundombinu muhimu kwa ajili ya kuinua elimu kwa wanafunzi wa eneo hilo.

Silinde alisema shule hiyo anaifahamu na atahakikisha anatoa msukumo wizarani ili fedha zitolewe za kufanyia marekebisho ya baadhi ya miundombinu inayohitajika na kujenga mipya kulingana na mahitaji yaliyopo.

Aliwapongeza wananchi wa mji wa Mbalizi kwa ushirikiano waliouonyesha kwenye ujenzi wa miundombinu hiyo huku akiwataka waendelee kushirikiana.

"Mji wa Mbalizi una mchango mkubwa sana kwenye maisha yangu ya elimu kwa sababu hata mimi nimesoma kwenye mji huu, nakuomba tu mheshimiwa mbunge uendelee kunikumbusha mara kwa mara jambo hili, lipo ndani ya uwezo wangu," alisema Silinde.

Aliwataka viongozi wa halmashauri kuhakikisha wanaendelea kusimamia ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha kwanza mwakani na kwamba serikali haitasita kuchukua hatua kwa watakaoshindwa kukamilisha ujenzi huo ifikapo Desemba 31, mwaka huu.



## Kura ya mapema imeleta mafanikio

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema utaratibu wa kura ya mapema uliotumika katika uchaguzi mkuu wa mwaka jana umeleta mafanikio makubwa na kukidhi malengo na matarajio ya watu ambao walikuwa hawapati nafasi katika siku ya uchaguzi mkuu kutumia haki ya demokrasia.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera na Uratibu wa Baraza la Wawakilishi, Dk. Khalid Salum Mohamed, aliyasema hayo jana wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Pandani, Prof. Omar Faki Hamad, aliyetaka kujua kura ya mapema imelalamikiwa na wananchi wengi na vyama vya siasa, hivyo serikali haioni kuja na haja ya kuondoa mfumo huo.

Dk. Khalid alisema kura ya mapema imepitishwa kwa mujibu wa Sheria ya Baraza la Wawakilishi ambayo lengo lake kubwa ni kutoa nafasi na fursa kwa watendaji wakiwamo wafanyakazi wa tume na wapigakura kutumia haki ya demokrasia kupiga kura kabla ya siku moja ya uchaguzi mkuu.

Alisema baada ya uchaguzi mkuu Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) hupokea taarifa ambazo zinatokana na waangalizi wa uchaguzi ambapo hakuna ripoti ya moja kwa moja iliyolalamika kuwapo kwa upungufu katika kura ya mapema.

Pia alisema ZEC iliwaandikia wadau na asasi za uchaguzi vikiwamo vyama vya siasa kutathmini uchaguzi mkuu na kuangalia sheria zake na kwamba hakuna asasi wala vyama vya siasa vilivyowasilisha malalamiko hayo.

Aidha, Dk. Khalid alisema milango ya tume ya uchaguzi iko wazi kwa ajili ya asasi za kiraia na vyama vya siasa kutoa maoni kuhusu maendeleo ya uchaguzi pamoja na sheria za tume ya uchaguzi kwa lengo la kuwa na uchaguzi utakaokwenda sambamba na mabadiliko ya demokrasia na utawala bora.

# Mabadiliko ya tabia nchi yatishia Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RIPOTI ya mazingira ya mwaka 2021/22 inaonyesha kwamba Zanzibar inakabiliwa na athari za mabadiliko ya tabia ya nchi na zaidi ya maeneo 148 yamevamiwa na maji ya bahari, hivyo kusababisha shughuli muhimu za wananchi hasa kilimo kutofanyika.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Saada Mkuya, alisema hayo jana wakati akiwasilisha taarifa ya hali ya mazingira inayotokana na mabadiliko ya tabia ya nchi kwa mwaka katika kikao cha Baraza la Wawakilishi.

Alisema maeneo 25 yameathirika kwa kuingiliwa na maji ya bahari kwa upande wa Unguja wakati kisiwa cha Pemba kikiongoza kwa zaidi ya maeneo 123.

Dk. Mkuya aliyataja maeneo yaliyoathirika ni katika sekta ya utalii, sekta ya uvuvi, chanzo vya majisafi na salama pamoja na makazi na miundombinu.

Alisema kwa mujibu wa utafiti uliofanywa wa mazingira na mabadiliko ya tabia ya nchi wa mwaka 2012 unaonyesha kwamba maeneo hayo yapo chini ya mita tano usawa wa bahari na kusababisha kina cha maji kupanda.

Uvamizi wa maji ya bahari yanayotokana na mabadiliko ya tabia ya nchi, alisema kwa kiasi kikubwa yanatishia mustakabali wa maendeleo ya sekta ya utalii kutokana na maeneo mengi ya fukwe kuvamiwa na bahari.

"Taarifa ya hali ya mazingira inaonyesha kwamba fukwe zetu ziko katika tishio la kutoweka kutokana na mabadiliko ya tabia ya nchi hasa kutokana na kasi ya maji ya bahari kuvamia maeneo ya fukwe ze za utalii," alisema.

"Hivi karibuni taasisi moja kutoka Marekani imeitaja Zanzibar kuwa nchi inayoongoza kwa kuwa na fukwe nzuri bora zenye kuvutia duniani hatua ambayo inakitangaza kisiwa kuwa bora katika sekta ya utalii," aliongeza.

Pia alisema mabadiliko ya tabia ya nchi yamesababisha athari kubwa katika sekta ya majisafi na salama kutokana na baadhi ya vyanzo vya maji kukauka pamoja na binadamu kufanya uharibifu wa ujenzi holela katika maeneo hayo.

Aliyataja baadhi ya maeneo ya ukanda jirani na bahari vyanzo vyake kuwapo katika tishio huku maji yake yakichanganyika na maji chumvi kiasi cha wananchi kushindwa kuyatumia maji hayo.

"Mabadiliko ya tabia ya nchi athari zake ni kubwa pamoja na vyanzo vingi vya maji kukauka kutokana na mabadiliko ya mazingira hatua ambayo inatishia mustakabali wa upatikanaji wa rasilimali hiyo kwa matumizi ya binadamu," alisema.

Dk. Mkuya aliwaambia wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba serikali imeanza kuchukua hatua mbalimbali kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia ya nchi ikiwamo kupanda miti aina ya mikoko kwa ajili ya kupambana na kasi ya mmomonyoko wa ardhi katika maeneo ya pembezoni mwa fukwe.

Alisema tayari wamevishawishi vikundi mbalimbali vya wanamazingira kupanda miti hiyo katika maeneo yaliyoko katika tishio la athari za mabadiliko ya tabia ya nchi ya kasi ya maji ya bahari kuvamia maeneo ya makazi ya wananchi.




Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wakifuatilia kikao cha baraza hilo Chukwani nje kidogo ya jiji la Zanzibar, jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Bilioni 50.6/- zatengwa kuwezesha wajasiriamali

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SHILINGI bilioni 50.6 zimetengwa kwa ajili ya uwezeshaji wananchi kiuchumi huku serikali ikiwa katika hatua za mwisho za kuwasilisha sheria ya kuiunganisha mifuko ya uwezeshaji kuwa na mfuko mmoja ili kuleta ufanisi.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Uchumi, Kazi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Pangawe, Ali Suleiman Ameir.

Katika swali hilo, Ameir alitaka kujua ufanisi wa mifuko ya uwekezaji katika kuwatumikia wajasiriamali kwa sasa maendeleo yake yakoje.

Soraga alisema kwa sasa serikali imechukuwa hatua tatu muhimu ikiwamo kutayarisha mwongozo wa uendeshaji wa mifuko hiyo pamoja na sera na baadaye sheria.

Alibainisha kuwa mchakato wa sheria bado unaendelea na utakapokamilika unatarajiwa kufikishwa mbele ya kamati ya sheria ya Baraza la Wawakilishi na baadaye kwenda kwa Baraza la Mapinduzi.

Soraga alisema hivi sasa kuna mifuko ya uwezeshaji wananchi kiuchumi saba ambayo imekuwa ikitoa mikopo yenye lengo la kupambana na hali ngumu ya maisha kwa wajasiriamali.

Aliitaja mifuko hiyo ukiwamo wa uwezeshaji wananchi ulioko chini ya tawala za mikoa na halmashauri za wilaya pamoja na mfuko wa uwezeshaji vijana ambao uko chini ya Wizara ya Habari na Vijana.

Pia alisema uko mfuko wa wajasiriamali wadogo ambao unafanya kazi katika mabaraza ya vijana yaliyoko katika mikoa ya Unguja na Pemba katika kuibua miradi mbalimbali ya uchumi.

Soagara alisema pia kuna mfuko wa kuwawezesha wajasiriamali katika kuendeleza viwanda vidogo vidogo Smida ambao huwasaidia wabunifu katika kuibuwa miradi ya kuwaendeleza.

Alisema serikali imetenga Sh. 50,636,032,910 kwa ajili ya kuwawezesha wajasiriamali wadogo 85,850 kupiga hatua kubwa ya maendeleo katika kazi za ubunifu wa miradi ya uzalishaji mali kiuchumi.

Kwa mujibu wa waziri, fedha hizo ni mkopo kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF) za ahuweni kupambana na ugonjwa wa corona ambazo kwa sasa kazi kubwa inayofanywa ni kuhakiki wajasiriamali watakaonufaika na fedha hizo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KIWANJA KIANUZWA.

KIWANJA KIANUZWA KISUSURU JKT KIWANJA KIPO KISUSURU JKT SEGEREA UKUBWA SQM 2252 KINA HATI BEI MILIONI 55, **KWA MAWASILIANO: 0786 857523 AU 0655 857523**

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
MOB: +255 - 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI



**BIBIANA LEOCADIUS NGOITANILE MWASAMILA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index **namba** S3794/0010 kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ya **NYANKUMBU GIRLS** mwaka **2015**, yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **MAD/P:25/VOL.V/234**

## KUPOTEA KWA CHETI



**MANJI MAKENE NYAKABI**
Anatangaza kupotea kwa cheti chake cha kidato cha nne index no **S0212-0001** kilichotolewa na Baraza la mitihani la Taifa kupitia Machame Secondary iliyopo Wilaya ya Hai Mkoa wa **Kilimanjaro Mwaka 1997**. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/577931/2021.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LUCY GODFREY NGALLAWA**

Anatangaza kupotea kwa kadi mbili za gari zenye reg.no t681adc/ Jina goodluck franciss imboma na reg t772adf/ Jina goodluck franciss imboma kwa yeyote atakeona au kuokota atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi **DOD/DOD/RB/529674/2021**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**Probate and Administration Cause**
**No……………………………………2021**
**In the Matter of the Estate of the late JACKSON CHELEYA MDOONONDO of Bwawani-Makulu, within Dodoma City**
**And**
**In the matter of application for letter of administration by JENIVA CHIMBWI MHAKA MDOONONDO**
**PETITION FOR LETTER OF ADMINISTRATION WHEN THE DECEASED DIED INTESTATE**
**(SECTION 56)**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 probate Rules GN NO. 369 OF 1963)**

ALL PERSONS Claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 5 Day of 1 / 2022

**Dated at Dodoma this 21 Day of 12/ 2021**

RESIDENT MAGISTRATE

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya Morogoro**
**Kituo cha Mjini Mkoa Wa Morogoro**
**Usimamizi wa Mirathi Na……336...2021**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU BOZEN JUMA ISMAIL MLAHI WA ……**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA APATAE BOZENI JUMA**

**TANGAZO**
(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 23 Mwezi 12 Mwaka 2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
- Endapo kuna yoyote mwenye wosia na marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia ya narehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika.

**Imetolewa Tarehe 16 Mwezi 12Mwaka 2021**

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

---

IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO
DISTRICT AT MOROGORO
PROBATE AND ADMINISTRATION
CAUSE NO 71 OF 2021

In the Matter of the Estate of the Late LAURENCE PAUL KUNAMBI

By 1. MARESERINA LAURENCE PAULO
2. ………………………………………………

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above –named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 1

RESIDENT MAGISTRATE

---

IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO
DISTRICT AT MOROGORO
PROBATE AND ADMINISTRATION
CAUSE NO 29 OF 2021

In the Matter of the Estate of the Late SENDORO JOHN KAVUTA

By 1.ELITWAZA JOHN KAVUTA
2. ………………………………………………

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above –named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 29 day of DEC…2021

Dated at D/COURT this 22 day of DEC …2021

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

IBRAHIM YERIKO MBILINYI anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya MITSUBISHI ROSA yenye namba za usajili T 197 DHV,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa MKB/RB/278/2021

---

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA BUSINESS REGISTRATION AND LINCESING AGENCY**
**Advertisement o Appointment of Liquidator**

**IN THE MATTER OF:** ZENNETH HR AND FINANCE SERVICES LIMITED
**Company Number:** 121475
**Of Address:** ILALA MCHIKICHINI, NHC BLOCK "C" HOUSE NO. 408, P.O.BOX 11008, DAR ES SALAAM, TANZANIA

That a Liquidator has been appointed to manage, control and sign on behalf of the company receive, collect and pay debts, and any other such incidental actions.

**Liquidator's name:** EMMANUEL WILLIAM KESSY

**Liquidator's Address:** MAKOA LAW CHAMBERS (ADVOCATES). 4", FLOOR IPS BUILDING, AZIKIWE STREET P.O BOX 71393 DAR ES SALAAM

**Date of appointment:** 5TH October 2021

**By whom appointment:** MEMBERS VOLUNTARY RESOLUTION

Any person with any claims or benefit owed to the above name company must, upon receiving 0-b, notice, contact the Liquidator at the address below;

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

CHARLES MGEMA LUBEJA anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya MAZDA DEMIO yenye namba za usajiili T 814 CEQ,yeyoye atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa DAR/URA/RB/593814/2021

## KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI

AVCO INVESTMENTS LTD

ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI

T350DAU-ARU/ARU/RB/596950/2021

T420DBY-ARU/ARU/RB/549728/2021

T446DBY-ARU/ARU/RB/549713/2021

YEYOTE ATAKAYEZIONA ATOE TAARIFA POLISI.

TAARIFA HIZI ZIMERIPOTIWA NA SAUMU MUSSA MBWANA

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# EAC wakutana kuamua mustakabali wa DRC

**Nairobi,** KENYA

WAKUU wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), wamekutana kwa njia ya mtandao, katika kikao chao cha 18 kisichokuwa cha kawaida kujadili masuala mbalimbali yanayohusu jumuiya hiyo, kikiongozwa na rais Uhuru Kenyatta, ambaye ndiye Mwenyekiti wa sasa.

Kikao hiki kimetanguliwa na kile cha mawaziri wanaohusika na jumuiya hiyo kutoka mataifa ya Kenya, Uganda, Tanzania, Burundi, Rwanda na Sudan Kusini.

Mambo mawili yanayojadiliwa na marais hao ni pamoja na kuingizwa kwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), kama mwanachama mpya wa Jumuiya hiyo, pia kubadilisha kanuni ya akidi wakati viongozi hao wanapokutana kujadili masuala yanayuhusu jumuiya hiyo.

Kanuni ya sasa kuhusu akidi, inaeleza kuwa mkutano wa viongozi hao unaweza kuendelea tu iwapo marais wote sita watakuwapo.

Katibu Mkuu wa Jumuiya hiyo, Dk. Peter Mathuki alisema kwamba kuingia kwa DRC, yenye watu karibu milioni 90 kwenye jumuiya hiyo, kutasaidia kupanua soko na fursa za kufanya biashara miongoni mwa nchi wanachama.

Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), inapakana na nchi tano za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), ambazo ni pamoja na Tanzania, Burundi, Rwanda, Uganda na Sudan Kusini.

**RFI**



Picha iliyopigwa angani ikionyesha magari yakielea na majengo kuzungukwa na maji, kutokana na mafuriko eneo la Shah Alam's Taman Sri Muda, nchini Malaysia, juzi. **PICHA: REUTERS**

## Kundi la waasi lakiri 'kupindua serikali'

**Kampala,** UGANDA

POLISI wa Uganda wanasema kundi jipya la waasi linalojulikana kwa jina la Uganda Coalition for Forces of Change, limeundwa nchini Uganda na kwamba hadi sasa wamewauwa maofisa wanne wa polisi na kuiba bunduki nne.

Operesheni iliyoendeshwa jana, imefanikisha kukamatwa kwa washukiwa nane na kupatikana kwa bunduki mbili katika Wilaya ya Kasanda kilometa 102, Magharibi ya jiji la Kampala.

Msemaji wa Polisi, Fred Enanga, alisema kuwa kundi hilo limekiri kuwa dhamira yao ni kupindua serikali.

Hata hivyo alisema uchunguzi unaendelea, ili kujua waanzilishi halisi wa kundi hilo jipya la waasi ni akina nani.

"Hadi sasa tumewakamata washukiwa nane ambao ni wanachama wa kundi jipya la waasi linalojulikana kama muungano wa vikosi vya Uganda kwa ajili ya mabadiliko.

Katika mashambulizi waliyofanya, maofisa wanne wa polisi waliuawa na bunduki zao kuchukuliwa.

Wamekiri kuwa mashambulizi dhidi ya polisi ni mkakati wa kupata bunduki na kulidhoofisha jeshi la polisi ambalo linaonekana kuwa kikwazo cha azma yao ya kubadilisha Serikali.

"Tumefanikiwa kupata bunduki 2 na risasi 22. Tutafanya uchunguzi mpana zaidi ili kujua ni viongozi gani wako nyuma ya kundi hili jipya na vitendo vyao vya uvunjaji sheria"

**BBC**

## Hamdok apanga kujiuzulu

**Khartoum,** SUDAN

WAZIRI Mkuu Sudan, Abdalla Hamdok ameliambia kundi la viongozi wa kitaifa wa kisiasa na wataalamu nchini humo kwamba, anapanga kujiuzulu katika muda wa saa chache zijazo.

Vyanzo viwili karibu na Hamdok vimeliambia shirika la habari la Reuters.

Awali vyanzo hivyo vilisema Waziri Mkuu huyo, angesalia madarakani iwapo tu atakuwa na uungwaji mkono wa kisiasa.

Hamdok alirejeshwa madarakani, Novemba 21, mwaka huu, kufuatia mapinduzi na jeshi lilichukua madaraka na kumaliza kipindi cha mpito cha ushirikiano na vyama vya siasa.

Licha ya baadhi ya wanasiasa kushiriki katika kuandaa mkataba wa kisiasa na jeshi, mkataba huo umekosolewa vikali na baadhi ya vyama vya kisiasa na wananchi.

Jumamosi, maelfu ya watu walifanya maandamano kuelekea Ikulu ya rais na kupinga utawala wa jeshi na uamuzi wa Hamdok kurudi madarakani.

**DW**



## Vikosi Ethiopia vyadai kuisafisha himaya TPLF

**Addis Ababa,** ETHIOPIA

SERIKALI ya Ethiopia, imesema jeshi lake lilikuwa likisafisha himaya za vikosi vya Tigray katika mikoa ya Kaskazini ya Amhara na Afar.

Habari hizo zinakinzana na taarifa za Wa-Tigray kwamba vikosi vyake vilijiondoa vyenyewe, ili kuweka mazingira mazuri ya kuleta amani.

Maelfu ya raia wameuawa kutokana na vita vya miezi 13 huku wengine 400,000 wakikabiliwa na hali ya ukame katika eneo la Tigray na watu milioni 9.4 wakihitaji msaada wa chakula kote Kaskazini mwa Ethiopia.

TPLF chama kinacho tawala Tigray, ambacho kipo vitani na serikali, kilitangaza kujitoa katika mikoa ya karibu ya Amhara na Afar, Jumatatu.

Msemaji wa serikali, Billene Seyoum aliwaeleza wanahabari katika mkutano kwamba kama ilivyo shuhudiwa katika wiki za hivi karibuni, vikosi vya taifa pamoja na vikosi shirika kutoka mikoa ya Afar na Amhara vimetwaa miji iliyokuwa inashikiliwa na TPLF.

**BBC**

## 64 wafariki ajali ya meli Madagascar

**Antananarivo,** MADAGASCAR

MELI ya mizigo ambayo haikuidhinishwa kusafirisha watu na kujaza kupita kiasi, imepata ajali baharini baada ya kujaa maji na kuua watu 64. Mamy Randrianavony, Mkurugenzi wa Operesheni za bahari kwenye shirika la Maritime and River Port (APMF), alisema maji yalijaa kwenye injini.

Ajali ilitokea Kaskazini-Mashariki mwa Madagascar na kwamba msako unaendelea kuwatafuta abiria 24 ambao hawajulikani walipo, shirika la usafiri wa majini, lilisema jana.

Watu 50 walionusurika walipatikana, shirika la Maritime and River Port, alisema.

Meli ilizama Jumatatu usiku, ikiwa na watu 138 kwa mujibu wa maelezo ya APMF.

**VOA**

# SIMBA QUEENS, RUVUMA KAMILI KUWANIA TAJI BARA

**Na Saada Akida**

SIMBA Queens inatarajia kuwakaribisha Ruvuma Queens katika mechi ya kufungua pazia ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Mo Simba Arena, Bunju nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kocha Mkuu wa Simba Queens, ambaye amejiunga na kikosi hicho hivi karibuni, Sebastian Nkoma, alisema ameiandaa vyema timu yake na anaamini ataondoka na ushindi kwenye mchezo huo wa kwanza.

Nkoma alisema wachezaji wote wako katika hali nzuri na wamejiandaa kuingia uwanjani wakiwaheshimu wapinzani wao kutokana na kuwafahamu vyema.

Kocha huyo alisema licha ya kuwapo na changamoto za kuondoka kwa wachezaji watano ndani ya kikosi cha timu hiyo, anaamini wachezaji waliobakia watajituma ili kufikia malengo ya kuzibakisha pointi tatu nyumbani.

"Mimi ni mgeni katika timu hii, pia kuna nyota watano ambao walifanikisha Simba Queens kupata ubingwa msimu uliopita hapo, hali hiyo itatufanya tuingie uwanjani kwa tahadhari kubwa sana ili kuhakikisha tunapata pointi zote tatu muhimu katika mchezo huo," alisema Nkoma.

Aliongeza anajua wapinzani wao wana kikosi imara, na ana imani mechi hiyo itakuwa na ushindani kwa sababu kila upande utahitaji kuanza msimu kwa kuondoka na matokeo chanya hasa wao ambao watakuwa wanatumia uwanja wa nyumbani.

"Kwa maandalizi tuliyofanya, tunaimani ya kufanya vizuri katika mchezo huo, kuhusu nyota wapya watatu waliosajiliwa hivi karibuni ambao ni Pambani Kuzoya , Barakat Olaiya na Sabinah Thom hawatakuwa miongini mwa kikosi kitakachocheza kesho (leo)," Nkoma alisema.

Aliongeza mbali na nyota hao wapya pia ataendelea kumkosa mchezaji wao, Asha Kadosho ambaye ni majeruhi ya muda mrefu kwa sababu hali yake bado haijaimarika sawa sawa.

Naye Kocha wa Ruvuma Queens, Manya Mkwenya, alisema wamejipanga vizuri kuhakikisha wanaanza vyema ligi hiyo kwa kuwafunga wenyeji Simba Queens na kurejea kwao na pointi tatu muhimu.

"Tumejiandaa vizuri kukabiliana na Simba Queens, tunajua ni timu nzuri, pia wao ndio mabingwa watetezi, tunaenda kucheza mechi hii kwa tahadhari kubwa ili kuhakikisha tunapata matokeo mazuri," alisema Mkwenya.

Mechi nyingine ya ligi hiyo itakayochezwa leo itakuwa ni kati ya Alliance Girls dhidi ya Mlandizi Queens kwenye Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza wakati kesho JKT Queens itawakaribisha Oysterbay Girls kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo.

Wenyeji Baobab Queens watacheza dhidi ya Yanga Princess kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma huku TSC Queens itawaalika The Tigers Queens kwenye dimba la CCM Kirumba, Mwanza na Ilala Queens itawafuata Fountain Gate Princess.

# Mshindi Mdundo DJ Battle atajwa

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Mdundo, ambayo inayoongoza kwa huduma za muziki mtandaoni Afrika, imemtangaza DJ Dully kuwa mshindi wa mpambano wa Ma-DJ (Mdundo DJ Battle) kwa mwaka 2021 na kumzawadia Sh. milioni saba.

Zawadi nyingine alizopata mshindi huyo ni muda katika mojawapo ya redio ili kuonyesha uwezo wake kwa kucheza DJ mix iliyompa ushindi.

Meneja Masoko Mwandamizi wa Kampuni ya Mdundo, William Abagi, alisema tayari mshindi huyo katika shindano hilo lililoshirikisha Ma-DJ zaidi ya 200 ameshakabidhiwa zawadi yake.

"Shindano hili limefanikiwa kwa kiasi kikubwa na ni la kwanza la aina hii kuendeshwa na Mdundo, kwa kweli tunashukuru mwitikio tuliouona. Tunatarajia kuendesha shindano la pili mwakani na matarajio ni kupata washiriki wengi zaidi kutoka sehemu mbalimbali nchini," alisema Abagi.

Aliongeza kampuni hiyo inafanya kazi na wasanii zaidi ya 100,000 Afrika na Tanzania ina watumiaji wengi zaidi wa huduma za Mdundo huku ikirekodi watumiaji maalumu milioni 4.1 katika robo ya mwaka katika kipindi kilichoanzia Septemba mwaka huu.

Mdundo imeshirikiana na Vodacom Tanzamia kuwapa nafasi wapenzi wa muziki kupata maudhui yenye hadhi ya Premium-kazi za Ma-DJ kwa gharama ya kuanzia Sh. 100 kwa siku.




Mwakilishi wa Kampuni ya Mdundo, Frida Mugarula (kulia), akimkabidhi hundi ya mfano mshindi wa shindano la Mdundo DJ Battle 2021, Abdul Mohamed 'DJ Dully' baada ya kutangazwa mshindi katika kinyang'anyiro hicho. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mayanga awaacha Mayele, Kagere

**Na Adam Fungamwango**

BAO lililofungwa dakika ya 13 na Vitalis Mayanga wa Polisi Tanzania katika mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Mtibwa Sugar kwenye Uwanja wa CCM Gairo, juzi limemfanya straika huyo kufikisha mabao matano.

Mayanga sasa amemfikia nyota, Jeremiah Juma wa Prisons lakini akiwaacha, Meddie Kagere wa Simba na Fiston Mayala wa Yanga, ambao kila mmoja amefunga mabao manne.

Katika mechi hiyo ambayo timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1, imemfanya Mayanga kufikisha mabao matano kama Jeremiah, na kufanya vinara wa kupachika mabao kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa kuna ni wazawa.

Alifunga mabao mawili Septemba 29, mwaka huu wakati Polisi Tanzania ikiichapa KMC mabao 2-0, akafunga bao pekee Oktoba 24, mwaka huu katika mechi waliyoshinda bao 1-0 dhidi ya Ruvu Shooting na goli lingine moja alilifunga Novemba Mosi, mwaka huu wakilazimishwa sare ya mabao 2-2 dhidi ya Mbeya Kwanza.

Wachezaji wenye mabao manne mpaka sasa ni wanne na kati yao, watatu ni wazawa ambao ni Feisal Salum wa Yanga, George Mpole (Geita Gold) na Reliants Lusajo wa Namungo huku mchezaji wa kigeni ni Mnyarwanda, Kagere.

## Nyota Simba SC akaribia KMC FC

**Na Adam Fungamwango**

KWA mara nyingine tena, kiungo mshambuliaji wa Simba, Ibrahim Ajibu anahusishwa na mchakato wa kujiunga na KMC kwa mkopo.

Habari za ndani kutoka kwenye klabu ya Simba zinasema wanatarajia kuwaacha baadhi ya wachezaji ambao mchango wao kwa timu hiyo ni mdogo wakati Ajibu akihusishwa kupelekwa KMC.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa KMC, Walter Harrison, alisema mpaka sasa hawajapokea ripoti yoyote ya usajili kuelekea dirisha dogo kutoka katika benchi lao la ufundi, lakini kama wakipata na jina la mchezaji huyo likiwamo, basi watalifanyia kazi.

"Kwa upande wetu hatujapokea ripoti ya mwalimu inayoeleza aina gani ya wachezaji ambao anawahitaji, kwa sasa, kama jina hilo linalotajwa litakuwamo ni moja ya majina waliorodhesha, tutalifanyia kazi ili kumpata, na kama ikishindikana kama mwanzo basi, " alisema ofisa huyo.

Alisema kutokana na mahitaji kidogo ya wachezaji, wana imani watakamilisha kila kitu kabla dirisha dogo halijafungwa.

"Hatutosajili wachezaji wengi, hatuna mahitaji makubwa sana, tunataka wachache tu wa kuongeza nguvu na hilo halitotupa tabu," alisema Harrison.

## ZISIKUPITE

### GOMEZ ANUKIA MADRID

REAL Madrid wanafuatilia hali ya mlinzi wa kati wa Liverpool na Timu ya Taifa ya England, Joe Gomez, ambaye ana umri wa miaka 24. ***(Mail)***

### COMAN AGEUKA LULU

MANCHESTER United, Barcelona na Real Madrid zote zinamwania winga wa Bayern Munich na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Kingsley Coman, mwenye umri wa miaka 25. ***(Mundo Deportivo)***

### LIVERPOOL YAMTAKA HAALAND

LIVERPOOL imeingia kwenye mbio za kuwania kumsajili straika wa Borussia Dortmund, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 21, ambaye ni raia wa Norway. ***(Sky)***

### MARTIAL AICHAGUA SEVILLA

FOWADI wa Manchester United na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Anthony Martial, mwenye umri wa miaka 26, anataka kujiunga na Sevilla kwa mkopo. ***(Sky Sports)***

### AZPILICUETA ATOA MSIMAMO

NAHODHA wa Chelsea, Cesar Azpilicueta mwenye umri wa miaka 32, anataka kubakia klabuni hapo licha ya Barcelona kuonyesha nia ya kutaka kumwongezea mkataba mara ule wa sasa utakapomalizika kipindi cha majira ya joto ***(The Athletic)***

### ALVAREZ ANUKIA UNITED

MANCHESTER United imewasiliana na River Plate juu ya uwezekano wa kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Argentina, Julian Alvarez, mwenye umri wa miaka 21 kwa dau la pauni milioni 17. ***(Ole)***

### SPURS, ROMA VITANI

KLABU ya Tottenham Hotspur na AS Roma zinawania kumsajili kiungo wa Hoffenheim na Timu ya Taifa ya Ujerumani, Florian Grillitsch, mwenye umri wa miaka 26. ***(Sky Sport)***

### UNITED SOKONI SERBIA

MANCHESTER United inafikiria kumsajili kiungo wa Lazio ambaye ni raia wa Serbia, Sergei Milinkovic-Savic, mwenye umri wa miaka 26. ***(Il Messaggero)***

### MARQUINHOS AKARIBIA CHELSEA

CHELSEA imeweka mezani ofa ya pauni milioni 72 kwa ajili ya mlinzi wa Paris St-Germain, Marquinhos mwenye umri wa miaka 27. ***(L'Equipe)***

### EVERTON KUJIIMARISHA

EVERTON itajaribu kwa mara ya tatu kumsajili mlinzi wa kulia wa Rangers na Timu ya Taifa ya Scotland, Nathan Patterson, mwenye umri wa miaka 20. ***(Guardian)***

### NEWCASTLE KUSAJILI SITA

NEWCASTLE inawania kusajili wachezaji sita, wakiwamo wawili kwa mkopo, wakati wa usajili wa dirisha dogo la Januari. ***(90min)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MARTIAL ACHAGUA KUELEKEA SEVILLA

Ni baada ya kuona nafasi ya kupata namba kwenye kikosi cha United...

**MANCHESTER, England**

MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Anthony Martial, amechagua kujiunga na klabu ya Sevilla ya nchini Hispania, kwa mujibu wa ESPN.

Mapema mwezi huu, wakala wa Martial aliweka wazi lengo la nyota huyo kutaka kuondoka Manchester United mapema wakati wa dirisha dogo la Januari litakapifunguliwa.

Lengo la kuondoka kwake ni kumpatia mchezaji huyo timu atakayopata nafasi ya kucheza mara kwa mara.

Tangu United imsajili Jodan Sancho, Cristiano Ronaldo, uwezo wa Marcus Rashford na Mason Greenwood, hivi vyote ni vikwazo kwa Martial ambaye hana namna ya kudumu kwenye kikosi hicho ambacho hata Edinson Cavani anapata shida kucheza mara kwa mara.

Kuporomoka kwa kiwango chake uwanjani, majeruhi ya mara kwa mara na mtindo wake wa maisha, vinatajwa kama vikwazo kwa mchezaji huyo kung'ara pale Old Trafford kwa misimu kadhaa sasa.

Licha ya Barcelona, Juventus na Newcastle United kutaka huduma ya Martial, ni Sevilla ndio imekuwa chaguo la mchezaji huyo.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, mshambuliaji huyo anaiona Sevilla ndio sehemu sahihi kwake kwa wakati huu na atafanya mazungumzo na kocha wa muda wa United, Ralf Rangnick kuhusu hatima yake ndani ya timu hiyo ndani ya siku chache zijazo.

MECHI KALI
HOME AWAY
AZAM
1.53 | 3.58 | 6.00
RUVU SHOOTING

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 804

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# NKETIAH AWASHUKURU WACHEZAJI ARSENAL



**LONDON, England**

MFUNGAJI wa mabao matatu, 'hat-trick', Eddie Nketiah, amewapigia saluti wachezaji wenzake baada ya kuiwezesha Arsenal kuifumua Sunderland kwenye robo fainali ya Kombe la EFL, juzi Jumanne.

Mchezaji huyo kijana alifunga mara tatu wakati washikabunduki hao wakifuzu nusu fainali ya kombe hilo kwa ushindi wa mabao 5-1 pale kwenye dimba la Emirates.

Nketiah alifunga bao la kwanza kwa kichwa akiunganisha mpira uliopigwa na Rob Holding kabla ya kufunga mengine mawili.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 sasa amefikisha mabao 10 katika mechi tisa alizocheza, saba zikiwa kwenye dimba la nyumbani.


Aliiambia Sky Sports baada ya mchezo huo: "Ni hisia nzuri sana kwangu. Napenda tu kuwashukuru wachezaji wenzangu.

"Nilipata asisti nzuri sana leo (juzi); nilichotakiwa ni kuwa tu katika sehemu sahihi.

"Ni jambo zuri kupata hat-trick yangu ya kwanza kwa timu ya wakubwa ya Arsenal.

"Haya ni mashindano ambayo mara zote nimekuwa nikipata nafasi ya kuanza na kupata nafasi kubwa zaidi ya kucheza."

# Xavi: Matokeo Barca yananinyima usingizi



**SEVILLE, Hispania**

XAVI alisema atapata wakati mgumu kuweza kulala baada ya Barcelona kushindwa kupata ushindi katika mchezo walioutawala na kulazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Sevilla hapo Jumanne.

Los Nervionenses walipata bao la utangulizi dakika ya 32, shukrani kwa mfungaji, Alejandro Gomez, lakini Barca walisawazisha kipindi cha pili kwa kichwa cha 'utata' cha Ronald Araujo.

Ulikuwa ni mchezo ambao Barca walistahili ushindi, kwani walipiga mashuti 15 katika kipindi cha kwanza - yakiwa mengi zaidi kuliko timu yoyote kwenye LaLiga msimu huu.

Jules Kounde alitolewa nje kwa kadi nyekundu dakika ya 64 baada ya kumrushia mpira usoni, Jordi Alba, lakini Barca walishindwa kutumia nafasi ya wapinzani wao kuwa pungufu.

Matokeo hayo yanamaanisha Blaugrana hao wameshinda mchezo mmoja tu kati ya nane ugenini, Xavi alionekana kuchanganyikiwa na matokeo hayo, kwani alitarajia kuondoka pale Andalusia akiwa na pointi zote tatu, huku akionyesha kuridhishwa na kiwango cha timu.

"Tumepoteza pointi mbili; tulistahili kushinda, hata wakati tulipokuwa 11 dhidi ya 11," alisema Xavi akiiambia Movistar.

"Itakuwa ngumu kwangu kulala kwa sababu tulitakiwa kushinda. Sevilla waliweza kutulia mchezoni na kuufanya sisi tuwe na wakati mgumu."

## HABARI MICHEZO

# PAWASA: SIMBA ITAFUTE MRITHI WA MIQUISSONE

**Na Dennis Fussi**

BEKI wa zamani wa Simba, Boniface Pawasa, ameishauri klabu hiyo kutafuta kiungo mshambuliaji aina ya Luis Miquissone, kipindi hiki cha usajili wa dirisha dogo.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam, Pawasa, alisema Simba kwa sasa wanahitaji kiungo mshambuliaji ambaye mwenye uwezo wa 'kusukumiza' mashambulizi mbele kwa kasi na kutengeneza nafasi nyingi za kufunga.

Amesema mchezaji aina ya Miquissone ndio haswa anayehitaji kwa sasa kwenye kikosi hicho cha Simba ambacho kinashika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kushuka dimbani mara tisa.

"Mimi kwa maoni na mtazamo wangu, Simba kwa sasa wanamhitaji zaidi kiungo mshambuliaji aina ya Luis Miquissone ili kuwasaidia zaidi kwenye mashambulizi," alisema Pawasa.

Aliongeza: "Kiungo mshambuliaji aina ya Misquison anaweza kuisaidia Simba inaposhambulia na hata wakati inapokosa umiliki wa mpira, kwani yeye anakuwa na haraka ya kuusaka mpira ulipo."

Alisema Simba kwa sasa hawatakiwi kuangalia zaidi sehemu nyingine kwa sababu pengo aliloacha Miquissone ndio 'kubwa zaidi' na linatakiwa kutafutiwa ufumbuzi wa haraka.

Pawasa ambaye ni Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa ya Soka la Ufukweni, alisema nafasi nyingine katika kikosi hicho cha mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara hazina tatizo kubwa ukilinganisha na pengo la nyota huyo kutoka Msumbiji.

Miquissone ambaye ni raia wa Msumbiji alisajiliwa na Al Ahly ya Misri baada ya kung'ara na Simba kwa kipindi cha misimu miwili aliyokaa nayo.



Mkufunzi wa kozi ya makocha wa watoto (Grassroot), Raymond Gweba (katikati), akiwaeleza jambo baadhi ya washiriki wa kozi hiyo inayoendelea kwenye Uwanja wa Karume Ilala, jijini Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mtibwa Sugar yajitetea kwa sare

**Na Dennis Fussi**

KOCHA wa makipa wa Mtibwa Sugar, Soud Slim, amesema sare waliyopata juzi Jumanne katika mchezo wa Ligi Kuu Bara dhidi ya Polisi Tanzania imetokana na kuwakosa wachezaji wao muhimu wa kikosi cha kwanza.

Mtibwa ilitoka sare ya bao 1-1 na Polisi Tanzania, mchezo uliopigwa kwenye Uwanja wa CCM Gairo, mkoani Morogoro ukiwa ni wa 10 na bado wanaendelea kuburuza mkia katika msimamo wa ligi wakiwa na pointi saba.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Slim alisema kama wangekuwa na wachezaji wao wote wa kikosi cha kwanza, anaamini wangepata ushindi katika mchezo huo.

"Mchezo wa leo (juzi) ulikuwa wetu na tungeweza kuibuka na ushindi kama tungekuwa na wachezaji wetu wote wa kikosi cha kwanza, lakini ndio hivyo tumeambulia pointi moja tu," alisema Slim.

Mtibwa Sugar, kabla ya mchezo huo iliiandika kwa Bodi ya Ligi kuomba kuahirishwa kwa mechi hiyo kutokana na wachezaji wake wengi wa kikosi cha kwanza kusumbuliwa na ugonjwa wa mafua.

Hata hivyo, bodi ilikataa ombo hilo kwa maelezo wachezaji waliobaki kikosini hapo walikuwa wanaweza kuendelea kucheza kwa sababu, kwa mujibu wa kanuni ya 30, idadi ya walikuwa wanaumwa haikufika zaidi ya nusu ya wachezaji wote.


4,667,160

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 26/12/2021 | 18:00 | Peterborough vs Reading | 2.37 | 3.28 | 2.84 |
| 02. 26/12/2021 | 18:00 | Millwall vs Swansea | 2.29 | 3.19 | 3.04 |
| 03. 26/12/2021 | 18:00 | Hull City vs Blackburn | 2.90 | 3.19 | 2.37 |
| 04. 26/12/2021 | 18:00 | Preston vs Sheffield Utd | 2.90 | 3.25 | 2.34 |
| 05. 26/12/2021 | 18:00 | Portsmouth vs Oxford Utd | 2.43 | 3.28 | 2.75 |
| 06. 26/12/2021 | 18:00 | Lincoln vs MK Dons | 2.89 | 3.29 | 2.32 |
| 07. 26/12/2021 | 18:00 | Cheltenham vs Plymouth | 2.99 | 3.33 | 2.24 |
| 08. 26/12/2021 | 18:00 | AFC Wimbledon vs Charlton | 2.70 | 3.24 | 2.50 |
| 09. 26/12/2021 | 18:00 | Dundee Utd vs Hibernian | 2.90 | 3.15 | 2.42 |
| 10. 26/12/2021 | 18:00 | Kortrijk vs Royal Antwerp | 2.75 | 3.55 | 2.43 |
| 11. 26/12/2021 | 18:00 | Burnley vs Everton | 2.48 | 3.15 | 2.95 |
| 12. 26/12/2021 | 18:00 | Inverness vs Partick Thisle | 2.33 | 3.23 | 2.89 |
| 13. 26/12/2021 | 18:00 | Hamilton vs Kilmarnock | 2.72 | 3.26 | 2.43 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 23 - DESEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1579 | Udinese Youth vs Cremonese Youth | 1.85 | 3.67 | 3.47 |
| 13:30 | 4581 | Gasogi United vs AS Kigali | 4.61 | 3.60 | 1.65 |
| 14:00 | 3138 | Mafra vs Moreirense | 2.84 | 3.13 | 2.34 |
| 15:00 | 1251 | Sebeta City FC vs Wolkite City FC | 3.22 | 2.79 | 2.32 |
| 15:00 | 3248 | KK Homeboyz vs Tusker | 2.07 | 3.04 | 3.47 |
| 15:30 | 3159 | Vietnam vs Thailand | 2.70 | 2.89 | 2.60 |
| 16:00 | 1397 | Geita Gold FC vs Tanzania Prisons | 2.20 | 2.76 | 3.54 |
| 16:00 | 3067 | Espoir FC vs Bugesera FC | 2.05 | 3.35 | 3.65 |
| 16:00 | 3212 | Kiyovu Sports vs Rutsiro FC | 1.57 | 3.90 | 6.00 |
| 16:00 | 4956 | OFI Crete vs Aris Salonica | 3.23 | 3.04 | 2.17 |
| 17:00 | 2185 | Hyderabad FC vs East Bengal | 1.65 | 3.66 | 4.53 |
| 17:00 | 4729 | Yeni Malatyaspor vs Kayserispor | 2.33 | 3.20 | 3.01 |
| 17:30 | 1924 | AL Khalidiyah vs Al Ahli Manama | 1.73 | 3.42 | 4.33 |
| 17:30 | 4256 | Inter Luanda vs Sporting de Benguela | 1.17 | 5.81 | 13.55 |
| 17:30 | 5514 | Porto B vs Penafiel | 2.38 | 3.28 | 2.79 |
| 18:00 | 2609 | Saint George FC vs Jimma Aba Jifar | 1.21 | 5.78 | 9.64 |
| 18:00 | 3621 | Kabuscorp Scp vs Wiliete SC | 2.90 | 3.20 | 2.50 |
| 18:00 | 4187 | Volos vs Panathinaikos | 2.89 | 3.23 | 2.25 |
| 18:00 | 4848 | Ionikos Nikea FC vs Lamia | 2.21 | 3.14 | 3.04 |
| 18:30 | 3404 | Mamelodi Sundowns vs Tshakhuma | 1.33 | 4.62 | 9.05 |
| 18:45 | 1797 | Teuta Durres vs Egnatia Rrogozhine | 1.49 | 3.61 | 6.55 |
| 18:45 | 5620 | Vllaznia vs Kukesi | 2.06 | 3.14 | 3.38 |
| 19:00 | 3382 | Azam vs Ruvu Shooting | 1.53 | 3.58 | 6.00 |
| 19:30 | 4811 | Hercules CF B vs UD Beniganim | 1.49 | 4.10 | 7.00 |
| 20:00 | 1941 | Maccabi Kishronot Hadera W vs Hapoel Raanana W | 1.36 | 5.00 | 6.15 |
| 20:00 | 2144 | Rio Ave vs Belenenses | 2.10 | 3.13 | 3.28 |
| 20:00 | 2965 | Besiktas vs Goeztepe | 1.61 | 4.05 | 4.84 |
| 20:00 | 4573 | Kifisias vs AEK Athens | 10.58 | 5.00 | 1.24 |
| 20:00 | 5499 | MS Kiryat Gat W vs AS Tel Aviv University W | 1.58 | 4.14 | 4.43 |
| 20:00 | 5616 | Mallorca B vs Inter Ibiza CD | 1.33 | 4.35 | 8.31 |
| 20:05 | 1385 | AL Badii vs Muharraq SC | 5.39 | 3.71 | 1.55 |
| 20:30 | 3934 | Orlando Pirates vs Amazulu | 1.37 | 4.23 | 8.86 |
| 20:30 | 5902 | Maccabi Bnot Emek Hefer W vs Hapoel Marmorek Rehovot W | 1.50 | 4.52 | 4.71 |
| 20:45 | 3443 | Anderlecht vs Kortrijk | 1.41 | 4.59 | 6.44 |
| 20:45 | 5765 | PSV Eindhoven vs GO Ahead Eagles | 1.11 | 7.87 | 18.69 |
| 21:00 | 2352 | FC Vilafranca vs UE Sants | 1.47 | 3.82 | 6.38 |
| 21:30 | 4064 | Bnot Netanya W vs Hapoel Beer Sheva W | 4.44 | 4.34 | 1.55 |
| 21:30 | 4562 | CE Manresa vs Hospitalet | 2.41 | 2.85 | 2.99 |
| 21:45 | 1368 | FC Vizela vs Sporting Braga | 4.04 | 3.51 | 1.76 |
| 21:45 | 2544 | Partizani Tirana vs KF Tirana | 2.41 | 2.85 | 3.00 |
| 22:00 | 1433 | Puente Genil vs Conil CF | 1.71 | 3.15 | 5.03 |
| 22:00 | 1729 | UE Castelldefels vs UE Vilassar De Mar | 2.68 | 2.82 | 2.68 |
| 22:00 | 2150 | CD Binisalem vs Felanitx | 1.47 | 3.80 | 6.35 |
| 22:00 | 3574 | Figueres vs UE Sant Andreu | 2.83 | 2.83 | 2.54 |
| 23:00 | 2696 | Brugge vs OH Leuven | 1.32 | 5.28 | 7.24 |
| 23:00 | 4044 | Sparta Rotterdam vs Waalwick | 1.76 | 3.49 | 4.43 |
| 23:00 | 4719 | UD Rotlet Molinar vs CD Murense | 1.78 | 3.13 | 4.53 |
| 23:45 | 1681 | Porto vs Benfica | 2.08 | 3.33 | 3.14 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Alhamisi Desemba 23, 2021
Nipashe



## Martial achagua kuelekea Sevilla



Wachezaji wa Simba wakiwasili kwenye Uwanja wa Ndege wa Tabora kwa ajili ya mechi ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara dhidi ya KMC itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani humo. **PICHA: SIMBA SC**

# SIMBA: TUMEFUATA POINTI TATU TABORA

## ●●●Msimbazi yapanga 'kushusha' kikosi tofauti katika mechi hiyo lakini...

**Na Saada Akida**

WAKATI nyota wa kimataifa wa Simba kutoka Uganda, Thadeo Lwanga akihusishwa na tetesi za kuachwa katika kikosi cha timu hiyo, uongozi wa mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara, umesema wako kamili na tayari kuwakabili KMC katika mechi ya ligi itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, Tabora.

Tayari kikosi cha Simba kilichoko chini ya Mhispania Pablo Franco, kimeshawasili Tabora tangu juzi kuendelea na maandalizi ya mchezo huo wa raundi ya tisa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Simba, Thierry Hitimana, alisema bado hali ya wachezaji wao haijaimarika vyema, lakini wanaendelea na maandalizi ya kuwakabili KMC katika mechi hiyo ya ligi.

Hitimana alisema licha ya changamoto hiyo ya kiafya waliyokuwa nayo, wana matarajio ya kwenda kutafuta matokeo chanya katika mchezo huo utakaochezwa kuanzia saa 10: 00 jioni.

"Hivi karibuni tumekutana na changamoto za maradhi lakini tunaendelea vizuri na tumesafiri salama hadi Tabora, na tuko tayari kwa ajili ya kupambana kutafuta matokeo chanya katika mchezo wetu huu muhimu,".

"Tumejiandaa vizuri licha ya kuwakosa baadhi ya nyota wetu kama John Bocco, Bernard Morrison na Erasto Nyoni ambao bado wanaumwa, habari nzuri ni kurejea kikosini kwa Rally Bwalya ambaye hakuwepo katika kikosi kilichoenda Kagera," alisema Hitimana.

Kocha huyo alisema kutokana na changamoto waliyokuwa nayo, wanatarajia kufanya mabadiliko katika kikosi chao kwa kutoa nafasi kwa wachezaji ambao hawakuonekana sana katika mechi zilizotangulia za timu hiyo ambayo bado inashiriki michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Aliongeza wanafahamu ligi hiyo imekuwa na ushindani na kwa sababu hiyo, kila mchezaji atakayepata nafasi ya kucheza atatakiwa kujituma na kupambana ili kufikia malengo.

"Tunaimani hadi kufikia Ijumaa wachezaji wetu watakuwa wameimarika zaidi, wanafahamu wanatakiwa kupambana ili kuvuna pointi, mechi haitakuwa nyepesi kwa sababu timu zote ni ngumu," Hitimana alisema.

Wakati huo huo, Kikosi cha Azam FC kinatarajia kuwakaribisha Ruvu Shooting katika mchezo mwingine wa ligi hiyo utakaochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, uliopo Chamazi nje kidogo ya jiji la Dar es Salaam.

Kocha Msaidizi wa Azam FC, Iddi Abubakar, alisema mchezo wao dhidi ya Ruvu Shooting utakuwa mgumu na wenye upinzani mkubwa kutokana na historia ya timu hizo mbili kila zinapokutana.

"Tumejiandaa vizuri kukabiliana na wapinzani wetu, tumefanyia kazi makosa yetu, na sasa tunaenda uwanjani kupambana na hatimaye kupata kile ambacho tunakitarajia ambacho ni pointi tatu," alisema Iddi.

Kwa upande wa Ruvu Shooting, Kocha Msaidizi, Mohammed Nakuchema, alisema watakuwa na mabadiliko makubwa ndani ya kikosi chao kwa sababu baadhi ya wachezaji ni wagonjwa na wengine wamekwenda katika kozi.

"Kutokuwepo kwa nyota hao hakutaathiri mipango yetu kwa sababu wachezaji wengine wapo na wako fiti kwa ajili ya kupambana dhidi ya Azam FC, tutazifuata pointi tatu," alisema Nakuchema.

Nahodha wa Ruvu Shooting, Renatus Ambrose, alisema wanaenda kupambana na 'kupigana' ili kujiweka katika nafasi nzuri katika msimamo wa ligi.

"Katika mechi iliyopita tumepata matokeo mabaya, kocha ameona makosa yetu na kufanyia kazi kuelekea mchezo wa kesho (leo), tumejiandaa vizuri na tutacheza kwa tahadhari kubwa kutokana na ubora waliokuwa nao wachezaji Azam FC,"alisema Ambrose.

## Nabi akamilisha hesabu za usajili

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema anaamini uongozi wa timu hiyo utahakikisha inawanasa nyota wote aliowapendekeza katika ripoti yake kuelekea dirisha dogo la usajili ambalo limeshafunguliwa ili kufikia malengo waliyojiwekea katika msimu huu wa 2021/22.

Nabi aliliambia gazeti hili usajili wake umeelekea katika maeneo muhimu mawili na analazimika kuimarisha idara hizo kutokana na 'mapengo' yalijitokeza baada ya kupata majeruhi.

Kocha huyo alisema anaamini kikosi chake kitaimarika zaidi na kuendelea kupata matokeo chanya katika kila mechi watakayocheza.

"Tunahitaji kushinda katika kila mechi iliyoko mbele yetu, tunatakiwa kujituma na kuonyesha kiwango kizuri ili kupata ushindi, tunajua ushindi pekee ndio siri ya kufikia mafanikio," alisema Nabi.

Aliongeza anafurahi kuona viwango vya wachezaji wake vinazidi kuimarika na kuongeza ushindani wa namba kwenye kikosi hicho.

Yanga imeweka wazi itasajili wachezaji wapya 'kimkakati' na si kukurupuka kwa sababu tayari ina kikosi imara ambacho kimeanza msimu vizuri.

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, aliliambia gazeti hili usajili wao katika kipindi hiki utakuwa ni wa kujaza nafasi ambazo zina mapungufu lakini pia wakiwapa mikataba mipya nyota ambao wanawahitaji.

"Tutaangalia wachezaji wapya na tutahakikisha tunawabakisha kwa kuwapa mikataba mipya wachezaji ambao bado tunawahitaji na wako kwenye mipango ya mwalimu," Bumbuli alisema.

Alisema kikosi chao kimesharudi jijini na leo kitaendelea na mazoezi kwa ajili ya kujiandaa kuikaribisha Biashara United katika mchezo wa Ligi Kuu utakaochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >